Pia ilielezwa kuwa ili kuongeza hamasa kwa wanachama katika uwekaji wa hisa, akiba na amana, uongozi uliandaa sera ya uhamasishaji wa hisa, akiba na amana, ambayo ilisomwa na kujadiliwa na wanachama na mwisho haikupitishwa na mkutano mkuu kwaajili ya uidhinishaji kabla ya kuanza kutumika mapema mwaka 2026.

NA	MABADILIKO	NYARAKA INAYOBADILIKA	INAVYOSOMEKA SASA	ITAKAVYOSOMEKA BAADA YA MABADILIKO
1	Kuanzisha utaratibu wa ajira za kudumu	SERA YA UTUMISHI	**Ukurasa Na. 7** **Kifungu 2:1** Makundi ya Watumishi katika UDOM SACCOS LTD: - **a. Watumishi wa Kudumu: -** Watumishi wa kudumu katika UDOM SACCOS LTD ni wale watakaoajiriwa na UDOM SACCOS LTD kwa mkataba wa kudumu wa miaka mitatu (3) na kulipwa mishahara na marupurupu yote yanayostahili mtumishi kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni hii. Watumishi katika kundi hili ni wafuatao katika UDOM SACCOS LTD: - 1. Meneja wa Chama. 2. Mhasibu. 3. Afisa Mikopo. 4. Mkaguzi wa Ndani. 5. Makarani wa Hesabu. 6. Mhudumu wa ofisi wa ndani 7. Afisa TEHAMA.	**Ukurasa Na. 7** **Kifungu 2:1** Makundi ya Watumishi katika UDOM SACCOS LTD: - **a. Watumishi wa Kudumu: -** Watumishi wa kudumu katika UDOM SACCOS LTD ni wale watakaoajiriwa na UDOM SACCOS LTD kwa mkataba wa kudumu, na kulipwa mishahara na marupurupu yote yanayostahili mtumishi kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni hii. Watumishi katika kundi hili ni wafuatao katika UDOM SACCOS LTD: - 1. Meneja wa Chama. 2. Mhasibu. 3. Afisa Mikopo. 4. Mkaguzi wa Ndani. 5. Makarani wa Hesabu. 6. Mhudumu wa ofisi wa ndani 7. Afisa TEHAMA.
		SERA YA UTUMISHI	**Ukurasa Na.13** **3:0 KADA ZA WATUMISHI** WATAKAOAJIRIWA NA UDOM SACCOS LTD– IDADI, MUDA WA AJIRA NA SIFA NA MGAWANYO WA KAZI. 1) Chama kitaajiri watumishi wafuatao kwa masharti ya kudumu yasiyozidi miaka 3 kama ifuatavyo: - i. Meneja wa Chama (1) ii. Mhasibu (1)	**Ukurasa Na.13** **3:0 KADA ZA WATUMISHI** WATAKAOAJIRIWA NA UDOM SACCOS LTD– IDADI, MUDA WA AJIRA, SIFA NA MGAWANYO WA KAZI. 1) Chama kitaajiri watumishi wafuatao kwa masharti ya mkataba wa ajira ya kudumu: - i. Meneja wa Chama (1) ii. Mhasibu (1) iii. Afisa Mikopo (3) iv. Mkaguzi wa Ndani (1)

			iii. Afisa Mikopo (3) iv. Mkaguzi wa Ndani (1) v. Karani wa Hesabu (1) vi. Mhudumu wa ofisi (1) vii. Afisa TEHAMA (1)	v. Karani wa Hesabu (1) vi. Mhudumu wa ofisi (1) vii. Afisa TEHAMA (1)
		SERA YA UTUMISHI	**Ukurasa Na.14** **3:2:2 SIFA ZA WATUMISHI "QUALIFICATION"** 7. Mkaguzi wa ndani **Kiwango cha Elimu** Shahada au Stashahada ya juu au Stashahada/shahada ya uzamili au CPA(T) atapewa kipaumbele	**Ukurasa Na.14** **3:2:2 SIFA ZA WATUMISHI "QUALIFICATION"** 7. Mkaguzi wa ndani **Kiwango cha Elimu** Shahada au Stashahada ya juu au shahada ya uzamili. Pia atapaswa awe na CPA(T)
			Ukurasa Na.22 **Kima cha chini na cha juu cha mishahara ya watumishi wa Chama: -** **6. Mkaguzi wa ndani** UDMSS I 700,000/= UDMSS II 1,120,000/= UDMSS III 1,340,000/= UDMSS IV 1,560,000/= UDMSS V 1,780,000/= UDMSS VI 2,000,000/=	**Ukurasa Na.22** **Kima cha chini na cha juu cha mishahara ya watumishi wa Chama: -** **6. Mkaguzi wa ndani** UDMSS I 1,500,000/= UDMSS II 1,720,000/= UDMSS III 1,940,000/= UDMSS IV 2,140,000/= UDMSS V 2,360,000/= UDMSS VI 2,580,000/=

AGENDA NA.11: MENGINEYO

Mwenyekiti aliwakaribisha wanachama watoe mapendekezo au maoni yatakayohusu maendeleo ya chama, wanachama walijadiliana na kuishauri Bodi kufanya yafuatayo;

11.1 Kwa miaka ijayo mjadala wa makisio uanze kujadiliwa kwanza kabla ya Kwenda kwenye ajenda nyingine.

11.2 Huduma ya bima inayotolewa na chama haifanyi vizuri sana kwasababu kunawanachama wengine wanatoa huduma kama hiyo na wanajitangaza, hivyo Bodi iangalie namna ya kufanya maboresho

AGENDA NA.12: KUAHIRISHA MKUTANO

12.1 Mwenyekiti aliahirisha mkutano kwa kutoa shukrani kwa wajumbe kwa mahudhurio na michango yao ya mawazo mnamo saa 11:32 jioni.

.....
ERASMUS TANDIKE
Katibu

.....
LEONCE MUJWAHUZI
Mwenyekiti

AJENDA NA: 5

YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TATU WA MWAKA 2025

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA

(UDOM SACCOS LTD)

YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TATU WA MWAKA 2025

MIN.Na	SUALA	UTEKELEZAJI	HATUA
13.6.6	Kuongeza riba juu ya amana maalumu kutoka 6% hadi 8%	Riba juu ya Amana imeongezeka kutoka 6% hadi 8% kama mkutano mkuu wa 13 ulivyo azimia.	Kwa taarifa
1	Wanachama watakao ruhusiwa kuingia kwenye mkutano mkuu ni wale walio maliza Hisa za lazima tu. Na wasipewe huduma yoyote hadi wakamilishe hisa zao	Wanachama wasiokamilisha hisa za lazima hawataruhusiwa kushiriki mkutano mkuu wa 14 wa mwaka 2026, kama mkutano mkuu wa 13 ulivyoazimia.	Kwa taarifa
3	Kuanzishwa kwa huduma ya mkopo wa bima	Huduma ya mkopo wa bima imekwisha anza kutolewa kama mkutano mkuu wa 13 ulivyo azimia.	Kwa taarifa
4	Katika kusherekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwa UDOM SACCOS LTD, bodi inapendekeza kufanyika kwa bonanza kwa kutumia kifungu cha elimu kwa wanachama.	Bonanza la kusherehekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwa UDOM SACCOS LTD limekwisha fanyika, na fungu la elimu lilitumika kama mkutano mkuu wa 13 ulivyo azimia.	Kwa taarifa
5	Kutoa Honoraria kwa wajumbe wa Bodi na kamati ya usimamizi wanao maliza muda wao.	Honoraria kwa wajumbe wabodi na kamati ya usimamizi imekwishatolewa kama mkutano mkuu wa 13 ulivyo azimia.	Kwa taarifa
6	Kununua viyoyozi kwa ajili ya ofisi ya chama	Linategemewa kutekelezwa kabla ya mwezi Disemba mwaka 2026	Kwa taarifa
7	Wanachama wote waliochelewesha na wanadaiwa marejesho ya nyuma, wapelekwe kwa waajiri wao ili kuhakikisha fedha hizo zinarudi.	Ofisi iliwasiliana na mwajiri (UDOM) na makubaliano yaliyofikiwa ni kuwaandikia barua wadaiwa wote. Barua ziliandikwa na kuziwasilisha masijala za kila kituo wakwapuaji wanapofanyia kazi, tatizo ni wadaiwa kutotoa ushirikiano wa kuja kuchukua barua hizo.	Kujadili
8	Kifungu cha michango kwa jamii itengewe kifungu chake na iwe tofauti na sherehe za ushirika	Kifungu cha michango kwa jamii kimetenganishwa na sherehe za ushirika kama mkutano mkuu wa 13 ulivyo azimia.	Kwa taarifa

AJENDA NA: 6

TAARIFA YA UKAGUZI WA NJE YA MWAKA 2025 (COASCO)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA
(COASCO)

TAARIFA YA WAKAGUZI NA TAARIFA ZA FEDHA ZA UDOM SACCOS LTD KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2025

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika
(COASCO)
Barabara ya Hatibu
S.L.P. 761
Simu: (026) 2323265, 2321485
Mkurugenzi Mkuu (026) 2321704
Mkurugenzi wa Ukaguzi (026) 2322050
Mkurugenzi wa Fedha na Utawala (026) 2321605
Mkurugenzi wa Utafiti na Ushauri (026) 2321671
Fax Na: 0262321486
Email: info@coasco.go.tz
DODOMA
TANZANIA

JUNI, 2026 ***ROA/UDOM SACCOS LTD/2025***

YALIYOMO

Maelezo	Ukurasa
Maelezo ya Awali	1
Taarifa Huru ya Wakaguzi.....	2 - 5
Takwimu za Chama	6 - 7
Taarifa za Chama.....	8
Taarifa ya Wajumbe wa Bodi	9 - 15
Tamko la Mkuu wa Idara ya Uhasibu.....	16
Taarifa ya Hali ya Fedha	17
Taarifa ya Mapato na Matumizi	18
Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji	19
Taarifa ya Mtiririko wa Fedha	20
Majedwali ya Ufafanuzi wa Taarifa za Fedha	21 - 31

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)Tanzania Bara

(Lilianzishwa kwa kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na.15 ya mwaka 1982) Kifungu cha 4(1)(a) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na.15 ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2005 kinaipa COASCO Mamlaka ya kuvikagua Vyama vya Ushirika.

Dira

Kuwa kituo cha kipekee cha utoaji huduma bora za ukaguzi na ushauri wa Vyama vya Ushirika katika Mashariki mwa Afrika.

Dhima

Daima kuendelea kutoa huduma bora ya ukaguzi na ushauri kuongeza utawala bora kwa wateja.

Miiko inayoongoza Shirika kuelekea kwenye Dira yetu na kusaidia kufanikisha Dhima yetu ni kama ifuatavyo:

(i) Kufuata maadili ya taaluma
(ii) Kuzingatia ubora na utoaji huduma haraka
(iii) Kutopendelea, Ushirikiano na Moyo kwa kufanyakazi pamoja
(iv) Elimumwendo na Uvumbuzi
(v) Kutokuwa na ubaguzi wa kijinsia

Tunafanya haya kwa:

- Kuchangia katika Usimamizi bora wa fedha za Umma kwa kuhakikisha kwamba wateja wetu wanawajibika kwa rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuboresha ubora wa huduma za Umma kwa kusaidia uvumbuzi katika matumizi ya rasilimali za Umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wateja wetu juu ya mapungufu yaliyopo katika mifumo ya utendaji;
- Kuwashirikisha wateja wetu katika mchakato na mzunguko wa ukaguzi; na
- Kuwapatia wakaguzi wetu vitendea kazi vya kutosha na vifaa vinavyowafanya wawe huru.

KAULI MBIU

Daima Kauli Mbiu yetu ni *"COASCO kwa Ukaguzi na Usimamizi bora wa Ushirika"*

TAARIFA HURU YA MKAGUZI KWA WANACHAMA WA CHAMA CHA USHIRIKA UDOM SACCOS LTD

Ripoti Inayohusu Taarifa za Fedha kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 31.12.2025

Hati Inayoridhisha

Tumekagua taarifa za fedha za **UDOM SACCOS LTD**, ambazo zinajumuisha taarifa ya hali ya fedha ya tarehe 31 Disemba, 2025, na taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya mabadiliko ya mtaji na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, na maelezo ya ufafanuzi wa taarifa za fedha, kujumuisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu.

Kwa maoni yetu, taarifa za fedha zilizoambatanishwa zinaonesha hali halisi ya fedha ya Chama cha Ushirika ya tarehe 31 Disemba, 2025, na matokeo ya shughuli zake pamoja na mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha.

Msingi wa Maoni

Ukaguzi wetu ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa. Wajibu wetu chini ya hivyo viwango umeelezwa katika aya ya wajibu wa mkaguzi kwa taarifa za fedha ya taarifa yetu. Tuko huru kulingana na matakwa ya maadili yanayohusiana na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha Tanzania, na tumetimiza wajibu wetu mwingine wa maadili kulingana na matakwa haya. Tunaamini ushahidi wa ukaguzi ambao tumeupata unatosheleza na unafaa kwa ajili ya msingi wa hati inayoridhisha.

Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Masuala muhimu ya ukaguzi ni yale kwa ukadirifu wa taaluma yalikuwa muhimu zaidi katika ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka huu. Masuala haya yalielezwa katika muktadha wa ukaguzi wetu wa taarifa za fedha kwa ujumla, na katika kutoa maoni yetu juu yake, hatutoi maoni tofauti katika masuala haya.

Taarifa Nyingine

Uongozi wa Chama unawajibika kwa ajili ya taarifa nyingine. Taarifa nyingine ni pamoja na taarifa ya Wajumbe wa Bodi na Tamko la Mkuu wa Idara ya Fedha lakini hazijumuishi taarifa za fedha na taarifa yetu ya ukaguzi.

Maoni yetu juu ya taarifa za fedha hayahusishi taarifa nyingine na hatutoi uthibitisho wa aina yoyote juu yake. Ukiunganisha na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha, wajibu wetu ni kusoma taarifa nyingine na kwa kufanya hivyo, tunaangalia kama taarifa nyingine kwa kiasi kikubwa haziendani na taarifa za fedha au uelewa wetu tulioupata wakati wa ukaguzi, ama vinginevyo zinaonekana kupotoshwa.

Iwapo, kutokana na kazi tuliyoifanya kuhusu taarifa nyingine itabainika kwamba kuna upotoshaji wa taarifa hizi nyingine, tunatakiwa kutoa taarifa juu ya ukweli huo. Hatuna jambo la kutolea taarifa kuhusu suala hili.

Wajibu wa Bodi ya Chama cha Ushirika

Bodi ya Chama cha Ushirika inawajibu wa kutayarisha na kuwasilisha taarifa hizi za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013. Vilevile bodi inawajibu wa kuweka mfumo wa udhibiti wa ndani ambao bodi inaona ni muhimu katika kutayarisha taarifa za fedha ambazo hazina dosari kubwa zinazotokana na udanganyifu au makosa ya kawaida.

Katika kutayarisha taarifa za fedha bodi inawajibu wa kutathmini uwezo wa Chama kuwa endelevu, ikionesha, kadri inavyofaa, mambo yanayohusiana na Chama kuwa endelevu na kutumia msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu isipokuwa ama bodi inakusudia kukifilisi Chama au kusitisha shughuli au hakina njia mbadala ya kweli isipokuwa kufanya hivyo.

Wajibu wa Mkaguzi

Shabaha yetu ni kupata uhakika wa maana kama taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina upotoshaji mkubwa, ama kwa sababu ya udanganyifu au makosa ya kawaida, na kutoa taarifa ya mkaguzi ambayo inajumuisha maoni yetu. Uhakika wa maana ni kiwango cha juu cha uhakika, lakini siyo dhamana kwamba ukaguzi uliofanyika kulingana na viwango vya ukaguzi vya kimataifa kila mara utagundua upotoshaji mkubwa unaokuwepo. Upotoshaji unaweza kutokana na udaganyifu au makosa ya kawaida na unafikiriwa kuwa mkubwa kama, peke yake au kwa ujumla, ungeweza kuathiri maamuzi ya watumiaji kwa msingi wa taarifa hizi za fedha.

Vilevile, kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 kinatutaka tujiridhishe kama shughuli za Chama cha Ushirika zimefanyika kulingana na matakwa ya Sheria au la na, kama vitabu na hesabu za Chama vina kubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama.

Kama sehemu ya ukaguzi kulingana na Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa, tunatumia maamuzi ya weledi na tunadumisha weledi kwa kushuku wakati wote wa ukaguzi. Pia:

- Tunatambua na kutathmini hatari za upotoshaji mkubwa wa taarifa za fedha, ama kutokana na udanganyifu au makosa ya kawaida, kupanga na kufanya ukaguzi kuitikia hatari hizo, na kupata ushahidi unaotosheleza na kufaa kwa ajili ya msingi wa maoni yetu. Hatari ya kutogundua upotoshaji mkubwa unaotokana na udanganyifu ni kubwa kuliko hatari inayotokana na makosa ya

kawaida, kwa sababu udanganyifu unaweza kuhusisha njama, kughushi, kuondoa taarifa kwa makusudi, mawasilisho yasiyo sahihi, au kupuuza mfumo wa udhibiti wa ndani.

- Kupata ufahamu wa udhibiti wa ndani kuhusiana na ukaguzi ili kupanga njia za ukaguzi ambazo zinafaa, lakini siyo kwa makusudi ya kutoa maoni juu ya kufaa kwa udhibiti wa ndani wa Chama.

- Kutathmini kufaa kwa sera za uhasibu zinazotumika na usahihi wa makadirio ya uhasibu na maelezo bayana yaliyofanywa na uongozi.

- Kuhitimisha kufaa kwa matumizi ya bodi juu ya msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu na, kwa kuzingatia ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, ama kuwepo kwa mashaka makubwa kuhusiana na matukio au hali inayoweza kuleta mashaka makubwa juu ya uwezo wa Chama kuendelea kuwa endelevu. Kama tunahitimisha kwamba yapo mashaka makubwa, tunatakiwa kuvuta nadhari katika taarifa yetu ya ukaguzi kuhusiana na maelezo bayana katika taarifa za fedha au, kama maelezo hayo hayatoshelezi, tubadilishe maoni yetu. Hitimisho letu limejengwa juu ya ushahidi wa ukaguzi tulioupata hadi kufikia tarehe ya taarifa yetu ya ukaguzi. Hata hivyo, matukio au hali za siku za usoni zinaweza kusababisha Chama kukoma kuendelea kuwa endelevu.

Tunawasiliana na Bodi ya Chama cha Ushirika kuhusiana, miongoni mwa mambo mengine, mawanda yaliyopangwa na muda wa ukaguzi na matokeo makubwa ya ukaguzi, kujumuisha mapungufu yoyote makubwa katika udhibiti wa ndani ambayo tunayabaini wakati wa ukaguzi wetu.

Pia tunatoa taarifa kwa Bodi ya Chama cha Ushirika ya kwamba tumefuata matakwa ya miiko ya kuwa huru, na tunawasiliana nao kuhusu mahusiano na mambo mengine yote yanayoweza kufikiriwa kukiuka uhuru wetu na pale inapobidi jinsi ya kuulinda.

Ripoti Inayohusu Matakwa Mengine ya Kisheria na Usimamizi

Kulingana na matakwa ya kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, tunatoa taarifa kwa maoni yetu kwamba:

a) Vitabu vya hesabu vilivyotunzwa na Chama vinakubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama; na

b) Shughuli za Chama zimefanyika kulingana na madhumuni ya Chama, Masharti na maamuzi yaliyofanyika katika mkutano mkuu wa Chama.

SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA
(COASCO)

CPA G.W.Kajaba
ACPA-PP 2191
Kny: KAIMU MKURUGENZI MKUU

Barabara ya Hatibu
DODOMA

CO-OPERATIVE AUDIT & SUPERVISION
CORPORATION
P. O. Box 761
DODOMA

Tarehe: 25/06/2026

NAKALA: Mrajis wa Vyama Vya Ushirika,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
S.L.P. 261, **DODOMA.**

TAKWIMU ZA CHAMA KUISHIA TAREHE 31.12.2025					
				31.12.2025	31.12.2024
A	Wanachama	HAI	ME	601	608
			KE	378	396
				979	1004
B	**Financial**			TSHS	TSHS
	Jumla ya Mali			6,836,247,592	6,326,341,367
	Mawekezo ya Wanachama			4,591,835,421	4,399,462,333
	Mikopo kwa wanachama			6,322,513,776	6,152,736,259
	Mtaji Tete (Core capital)			1,352,441,556	1,104,385,943
	Hisa za wanachama			858,539,204	642,219,689
	Mtaji halisi wa chama(Institutional Capital)			493,902,353	462,166,254
	Jumla ya Mapato			837,799,479	799,715,575
	Jumla ya riba ya mkopo			220,000,000	733,921,185
	Jumla ya Matumizi			530,408,896	505,628,376
	Wafanyakazi	Kudumu	M	2	2
			F	3	3
				5	5
C	**Uwiano**				
(i)	**Uwiano toshelezi**				
	Mtaji tete/Jumla ya mali			20%	17%
	Mtaji/Mawekezo ya wanachama			29%	25%
	Mtaji halisi wa chama/Jumla ya mali			7%	7%
(ii)	**Uwiano na Ukwasi (15%)**				
	Fedha taslim+Mawekezo ya mda mfupi +Wadaiwa			616,369,642	-
	Akiba, Amana & Wadai wa mda mfupi			4,611,963,612	-
				13%	-

1. Mahitaji ya mtaji yanayoridhisha

Kuhakikisha kuwa chama cha kuweka na kukopa kinaendeleza mtaji unaotosheleza ili kulinda au kuweka tahadhari juu ya amana za wanachama pamoja na wadai dhidi ya hasara zinazotokana na athari za kibiashara ambazo chama cha kuweka na kukopa kinakabiliana nazo kifedha. Athari hizi ni pamoja na mikopo kutorejeshwa uwekezaji, mabadiliko ya sheria,ukwasi, kiwango cha riba na ushindani wa biashara. Hiki ndicho kipimo cha hali ya fedha ya Asasi. Mtaji unaotosheleza unahamasisha kujiamini katika Asasi.

2. Mtaji tete

Mtaji tete wa chama cha kuweka na kukopa ni jumuisho la hisa za wanachama, malimbikizo ya ziada matengo mengine ya mtaji pamoja na Ruzuku/michango kutoka katika Taasisi na wadau mbalimbali wa maendeleo.

FOMULA

Mtaji tete = Hisa za wanachama + malimbikizo ya ziada + Matengo ya mtaji + Ruzuku/misaa

3. Mtaji halisi wa Asasi

Mtaji halisi wa Asasi ni sehemu ya mtaji tete ambayo inabaki kuwa mali ya Asasi ambayo hakuna mwanachama anayedai

FOMULA

Mtaji halisi = Mtaji tete - Hisa za wanachama.

4. Ukwasi

Ukwasi = Fedha taslimu na usawa

TAARIFA MUHIMU ZA CHAMA

WAJUMBE WA BODI WALIOHUDUMU KUISHIA 31.12.2025

NA	JINA LA MJUMBE	CHEO
1	Dr. Leonce Mujwahuzi	Mwenyekiti
2	Dr. Andwele Mwakasege	M/Mwenyekiti
3	Dr. Leonard Katalambula	Mjumbe
4	Sarah Kato	Mjumbe
5	Imani Haule	Mjumbe
6	Monica Nnko	Mjumbe
7	Ndalahwa Gedela	Mjumbe

Eneo la Biashara
Ofisi za chama: Chuo kikuu cha Dodoma
Jina la chama: UDOM SACCOS Ltd
S.L.P 2765
Reg Na. DOR 715
Telephone no: +255 767 561 854
Email : udomsaccos@gmail.com

Taarifa za Benki
CRDB Benki PLC
A/c no. 01J1383827500
NMB Benki PLC
A/c no. 52010035403
EXIM Benki PLC
A/c no. 0350002288

Mkaguzi
COASCO
P.O BOX 761
DODOMA

TAARIFA YA WENYE MAMLAKA KUISHIA TAREHE 31.12.2025

Bodi ya UDOM SACCOS LTD inatoa taarifa yake kuhusiana na hesabu zilizo andaliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31.12.2025 ambayo inaonesha hali ya kiutendaji ya UDOM SACCOS Ltd. Bodi imejiridhisha pasi na shaka kuwa taarifa hizi za fedha zimeandaliwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa yaani (IFRSs).

1. UANDIKISHWAJI

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Chuo Kikuu cha Dodoma, kilianza mchakato mwaka 2009 wa uanzishwaji wake, mchakato huo ulikamilika na kuweza kupata usajiri mnamo tarehe 05/01/2011 na kupewa namba ya usajili DOR 715 kwa mujibu wa sheria Na.20 ya vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 ambayo kwa sasa imefanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013. Baada ya maboresho ya sheria za usimamizi wa vyama vya ushirika kwa sasa chama kinasimamiwa na sheria Na. 10 ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018 hivyo kilisajiliwa upya tarehe 04/07/2023 na kupewa namba ya usajili PRI-DOM-DOM-CC-2022-130. Chama kilianza kutoa huduma rasmi mwaka 2013 baada ya kupata viongozi wake kwa mujibu wa taratibu za uchaguzi wa vyama vya Ushirika, chini ya sheria ya vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2019.

2. DIRA-(VISION)

Dira ya UDOM SACCOS LTD ni Kuwa chama bora cha ushirika wa akiba na mikopo kinachoongoza kwa utoaji wa huduma bora, bunifu, na endelevu za kifedha kwa wanachama wake katika sekta ya elimu na taaluma.

3. DHIMA - (MISSION)

Dhima ni Kutoa huduma jumuishi, salama, na zenye tija za kifedha kwa wanachama wa sekta ya elimu na taaluma kwa kutumia mifumo bora ya usimamizi, teknolojia ya kisasa, na maadili ya uadilifu, uwazi, na uwajibikaji.

4. CHOMBO CHA JUU CHA MAAMUZI

Chombo cha juu cha maamuzi ya UDOM SACCOS LTD ni Wanachama kwa umoja wao wanapokua katika Mkutano Mkuu. Kila mwaka wanachama wa UDOM SACCOS LTD hufanya Mkutano mkuu ili kupokea, kujadili na kupitisha taarifa, mipango, sera na taratibu mbalimbali, pamoja na kuidhinisha mapato na matumizi kwa mwaka husika.

5. WAJUMBE WA BODI

Wajumbe wa Bodi ya UDOM SACCOS LTD ambao wameiongoza UDOM SACCOS LTD katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025 ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo: -

Na	Jina	Wadhifa	Uraia	Tarehe Ya Kuchaguliwa	Tarehe Kujiuzu
1.	Dr.Leonce Mujwahuzi	Mwenyekiti	TZ	2024	2026
2.	Dr. Andwele Mwakasege	M/Mwenyekiti	TZ	2024	2026
3.	Dr. Leonard Kamanga	Mjumbe	TZ	2024	2026
4.	Sarah Kato	Mjumbe	TZ	2024	2026
5.	Monica Nnko	Mjumbe	TZ	2024	2026
6.	Imani Haule	Mjumbe	TZ	2024	2026
7.	Ndalahwa Gedela	Mjumbe	TZ	2024	2026

Wajumbe hao walikutana mara nane (8) katika mwaka huu na pia ilitoa taarifa yake katika Mkutano Mkuu wa wanachama wote uliofanyika tarehe 14/10/2025. Bodi hii imekuwa ikifanya shughuli zake kwa kuisimamia menejimenti ili kuhakikisha shughuli za chama zinakwenda kiufanisi na kufikia malengo yake.

Aidha UDOM SACCOS LTD ina kamati ya usimamizi iliyochaguliwa katika mkutano mkuu wa wanachama yenye wajumbe watatu (3), kama jedwali hapa chini linavyoonyesha:

Na	Jina	Wadhifa	Uraia	Tarehe Ya Kuchaguliwa	Tarehe Ya Kujiuzulu
1.	Emmanuel Kibulwi	Mwenyekiti	TZ	2024	2026
2.	Aquilina Nshalla	Katibu	TZ	2024	2026
3.	Asia Rubeba	Mjumbe	TZ	2024	2026

Wajumbe hao walichaguliwa na wanawajibika moja kwa moja kwa Mkutano Mkuu wa wanachama wote. Kamati hii ilikutana mara nne (4) katika mwaka huu na pia ilitoa taarifa yake katika Mkutano Mkuu wa wanachama wote uliofanyika tarehe 14/10/2025

6. UTAWALA BORA

Bodi ya UDOM SACCOS LTD inatekeleza wajibu wake kupitia kamati zake mbalimbli, pia Bodi ya UDOM SACCOS LTD imeajiri watendaji watano katika ngazi za Meneja, Mhasibu, Maafisa Mikopo wawili na Afisa TEHAMA. Watendaji hawa wanaisaidia Bodi kwa kiasi kikubwa kutimiza dira na dhamira ya Chama. Aidha, Bodi ya UDOM SACCOS LTD inao wajibu wa; -

6.1 Kusimamia shughuli za UDOM SACCOS LTD, kupanga, kuamua na kusimamia shughuli za uwekezaji na kuhakikisha kuwa inatambua maeneo yenye hatari kwa shughuli za UDOM SACCOS LTD.

6.2 Kupitia na kufanya tathmini ya Bajeti pamoja na mpango mkakati wa UDOM SACCOS LTD

6.3 Kuhakikisha kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani pamoja na sera madhubuti zina kuwapo na zinafuatwa kwa kuzingatia kanuni na misingi ya utawala bora.

UDOM SACCOS LTD inaendeshwa kwa kufuata misingi na kanuni ya utawala bora, na wajumbe wa Bodi wanatambua umuhimu wa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Kulingana na Masharti ya UDOM SACCOS LTD, Bodi inapaswa kukutana angalau mara nne kwa mwaka. Bodi imekasimu shughuli za kila siku za kiutendaji za UDOM SACCOS LTD kwa Meneja na Meneja huyo hualikwa kuhudhuria vikao vya Bodi ili kuwa kama kiungo kati ya menejimenti ya UDOM SACCOS LTD na Bodi, na pia Meneja ndiye anachukua nafasi ya Katibu wa Bodi.

Bodi ya UDOM SACCOS inakamati moja (1) ambayo ni Kamati ya mikopo. Na katika kuhakikisha utawala bora, kamati ya Mikopo inao wajumbe wafuatao kama ilivyooneshwa hapa chini.

Kamati ya mikopo inao wajumbe wafuatao; -

NA.	Jina	Nafasi	Uraia
1.	Sarah Kato	Mwenyekiti	TZ
2.	Monica Nnko	Katibu	TZ
3.	Ndalahwa Gedela	Mjumbe	TZ

Kamati hii hutoa taarifa kwa Bodi.Pia hukutana angalau mara moja kila mwezi kujadili maombi ya mikopo kwa wanachama na kwa dharura inaweza kukutana kila inapobidi.

7. MIKOPO KWA VIONGOZI NA WATENDAJI

Katika mwaka wa fedha 2025 jumla ya mikopo yenye thamani ya Tshs. 140,000,000/= ilitolewa kwa Viongozi, hadi tarehe 31 Desemba, 2025 bakaa ya mikopo kwa viongozi ni Tshs. 231,215,861/= ikiwa ni 4% ya mikopo yote kwa Wanachama na ubora wa mikopo hiyo ya Viongozi na Watendaji ni 100%.

8. MTAJI WA UDOM SACCOS LTD

Katika mwaka huu mtaji wa UDOM SACCOS ni shillingi za kitanzania 1,973,257,634 ambao unajumuisha Hisa, malimbikizo ya faida, Bima ya mikopo na matengo ya akiba mbalimbali za kisheria kama ifuatavyo: -

- Hisa Tshs. 858,539,204/=
- Malimbikizo ya ziada Tshs. 289,169,635/=
- Bima ya Mikopo Tshs. 211,350,640/=
- Matengo mbalimbali ya kisheria yana thamani ya jumla ya Tshs. 614,198,156/=

9. MENEJIMENTI

UDOM SACCOS LTD ina watendaji watano (5) kwa nafasi za Meneja, Mhasibu, Maafisa Mikopo wawili. Na Afisa TEHAMA Ambao hufanya kazi huku wakisimamiwa na Bodi ya chama kwa mujimu wa sheria na kanuni za vyama vya ushirika, sheria ya kazi ya Jamhuri ya muungano watanzania pamoja na kanuni na sera ya Ajira ya UDOM SACCOS LTD

Na	Jina	Wadhifa	Uraia
1.	Erasmus Tandike	Meneja	TZ
2.	Jestina Boniface	Mhasibu	TZ
3.	Yasinta Kanemela	Afisa Mikopo	TZ
4.	Atugonza Ishengoma	Afisa Mikopo	TZ
5.	Ericko Mwalongo	Afisa TEHAMA	TZ

10. WANAHISA

Wana Hisa wa UDOM SACCOS LTD ni wanachama wote ambao idadi yao ni Kama ifuatavyo:

UANACHAMA	2025			2024		
	ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA
HAI	562	363	925	586	393	979
SINZIA	39	15	54	22	3	25
JUMLA	601	378	979	608	396	1004

11. MIPANGO YA MAENDELEO YA BAADAE

UDOM SACCOS LTD itaendelea na mpango wa kuboresha na kuleta faida kwa njia ya kubuni huduma mbalimbali zenye manufaa kwa wanachama bila kutumia gharama kubwa na kwa kuzingatia hatari zinazoweza kujitokeza katika kuboresha shughuli hizo. Mipango iliyopo yenye kuleta huduma bora zaidi pamoja na kuongeza faida ni; kuhamasisha wafanyakazi wa chuo kikuu cha Dodoma ambao sio wanachama kujiunga na UDOM SACCOS LTD na, kuwahamasisha wanachama kuwa na tabia ya kuweka Amana sambamba na Akiba zao. Jambo lingine ni kufanya marekebisho ya masharti na sera mbali mbali ili kuruhusu wanachama kuweka Hisa zaidi na kubadilisha thamani ya Hisa ili kwenda na wakati wa sasa.

12. MATOKEO YA SHUGHULI ZA KIBIASHARA NA GAWIO

Katika mwaka huu chama hakikuweza kugawa gawio kwa wanachama wake licha ya taarifa ya mkaguzi wanje kuonesha faida iliyopatikana kuwa inatosha kufanya hivyo, sababu kubwa ya kutofanya hivyo ilikuwa ni kuweza kutunisha mfuko wa chama ili kuweza kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wanachama lakini pia chama kilitoa riba juu ya akiba kwa kiwango kikubwa lengo likiwa kuwamotisha wanachama kuweka zaidi akiba ili kurahisisha upatikanaji wa pesa za kukopesha.

13. HALI YA UTENDAJI KWA MWAKA HUU

Kulingana na taarifa ya hali ya kifedha pamoja na mapato na matumizi kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2025, hali inaonyesha kuwa urejeshaji wa mikopo ya wanachama ni mzuri kutokana na elimu iliyotolewa kwa wanachama juu ya ushirika, ujasiriamali, fedha na uwekezaji. Wanachama wengi wamekuwa wanakopa na kurejesha kwa wakati.

14. UDHIBITI WA HATARI NA MIFUMO YA NDANI

Bodi inatambua na kukubali wajibu wa kudhibiti majanga na hatari pamoja na udhibiti wa mifumo ya ndani ya UDOM SACCOS LTD. Ni kazi ya menejimenti kuhakikisha kuwa upo utoshelezi wa mifumo ya ndani ya udhibiti wa kifedha na ya shughuli za uendeshaji wa UDOM SACCOS LTD kuwa ni endelevu ili kuwa na uhakika kuhusiana na:

14.1 Kulinda mali za UDOM SACCOS LTD

14.2 Uendeshaji wa shughuli kwa wakati na gharama ndogo

14.3 Kufuata sheria na kanuni zinazohusika,

14.4 Uhakika wa utimilifu wa miamala ya kifedha na uwezo wa kuwa endelevu Katika shughuli za UDOM SACCOS LTD.

Bodi imetathmini udhibiti wa hatari na mifumo ya ndani kwa kupitia kamati ya usimamizi ya UDOM SACCOS LTD na kubaini kuwa mifumo iliyopo inatosheleza.

15. HALI YA UHAI WA SACCOS

Bodi inathibitisha kuwa kanuni za uhasibu na viwango vya kimataifa (IFRSs) katika kuandaa taarifa hizi zimefuatwa na katika kuhakikisha hali ya uhai na uendelevu wa UDOM SACCOS LTD. Bodi ina kila uthibitisho kuwa shughuli za UDOM SACCOS LTD zitakuwa na uhai endelevu kwa miaka ijayo hasa kwa kuzingatia kuwa UDOM SACCOS LTD inatengeneza Faida kila mwaka, ubora wa mikopo kwa Wanachama ni mzuri.

16. MAFUNZO

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025 Chama kilitumia kiasi cha shillingi 89,400,000/= kwa ajili ya mafunzo mbalimbali ya Wanachama, Watendaji na Bodi. Hii ni katika kuwaelimisha wanachama na kuboresha hali ya uongozi na utendaji katika SACCOS.Viongozi wa Bodi, kamati ya usimamizi na watendaji tayari wamekwishahudhuria mafunzo mbalimbali.

17. HALI YA USALAMA NA AFYA

Mazingira ya UDOM SACCOS LTD yanahakikishwa kuwa yapo katika hali ya usalama na kiafya kwa watumishi wote kwa ujumla. Hata hivyo chama kinawapatia wa watendaji wote huduma ya Bima ya Afya kwa kuwalipia 50% ya gharama za Bima ya Afya ili kuhakikisha hawapati tabu yoyote pindi wanapokuwa wagonjwa.

18. MISAADA YA KIFEDHA KWA WATUMISHI

UDOM SACCOS LTD katika masharti yake inaruhusu watendaji kuwa wanachama hivyo, hupewa stahiki za huduma za Chama kwa usawa na Wanachama wengine.

19. MPANGO WA MAFAO KWA WATUMISHI

UDOM SACCOS LTD imejiunga na NSSF kwa mpango wa mafao ya mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watendaji wake. Aidha, chama kimekuwa kikichangia 10% sawa na watendaji na kufanya jumla ya 20% ya watendaji na kuiwasilisha NSSF kila mwezi ikiwa ndio michango yao katika mfuko huo.

20. MAHITAJI YA SHERIA

UDOM SACCOS LTD inazingatia sheria za nchi kwa kulipa kodi stahiki, kufanya makato ya kodi za wafanyakazi na kuziwasilisha TRA, Chama kwa sasa hakichangii kodi ya SDL kwa kuwa kina watendaji watano (5) wakati sheria inataka wafanyakazi wawe 10.

21. MICHANGO YA HIARI KWA VYAMA VYA KISIASA NA KIJAMII

UDOM SACCOS LTD haijatoa michango yoyote kwa chama chochote cha siasa au vyama vya jamii vya hiari.

22. JUKUMU KWA JAMII

UDOM SACCOS LTD kwa mwaka wa fedha 2025 kimetoa mchango kwa jamii kwa kupeleka vifaa tiba pamoja na vifaa vingine vya matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Mlowa iliyopo Mlowa Bwawani.

23. WAJIBU WA BODI

Sheria ya ushirika inazitaka Bodi za vyama kuhakikisha kuwa hesabu za UDOM SACCOS LTD zinatayarishwa kwa kuonyesha hali halisi yake ya kifedha na kifaida au hasara kwa kila mwaka wa fedha. Pia inazitaka Bodi

kuhakikisha kuwa vitabu vinaandikwa kulingana na miongozo ya uhasibu iliyopo na kuonyesha hali halisi ya kifedha ya UDOM SACCOS LTD. Bodi inalo jukumu pia la kuhakikisha kuwa mali za chama zinalindwa na hakuna ubadhirifu wowote unaotokea katika mali za UDOM SACCOS LTD. Bodi inakubali jukumu hili na kubainisha kuwa hesabu hizi zimeandaliwa kwa kufuata miongozo ya uhasibu iliyopo sasa kama inavyotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA) ambayo ni IFRS.

24. SERA NA MIONGOZO

Chama kimeshatunga Sera za aina 17 ikiwa ni Sera ya uhasibu na Fedha, Sera ya Ukwasi mali na dhima, Sera ya utumishi, Sera ya Mikopo, Sera ya udhibiti majanga, Sera ya udhibiti wa fedha aharamu, Sera ya ukaguzi wa ndani, Sera ya ufuatiliaji madeni, Seara ya uhifadhi wa kumbukumbu, Sera ya ulinzi wa mlaji, Sera ya uwekezaji, Sera ya manunuzi, Sera ya mfuko wa majanga, Sera ya migogoro Sera ya Tehama, Sera ya mfuko wa maendeleo na Sera ya uuzaji mali. Pamoja na Sera hizo, chama pia kina Masharti ambayo ndio muogozo mama katika kukiendesha chama.

25. MKAGUZI

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) ndiyo Mkaguzi wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1)(a) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na. 15 ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2005 na kwa mujibu wa kifungu cha 55(3) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

Imeidhinishwa na Bodi ya UDOM SACCOS na kusainiwa kwa niaba ya Bodi na:

----------	24/06/2026 ----------
MWENYEKITI	TAREHE
----------	24/06/2026 ----------
MENEJA	TAREHE

TAMKO LA MKUU WA IDARA YA UHASIBU YA UDOM SACCOS LTD

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi kulingana na mamlaka iliyopewa chini ya Sheria ya Wakaguzi na Wahasibu (Usajili) Na.33 ya mwaka 1972 kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.2 ya mwaka 1995, inataka taarifa za fedha kuambatana na tamko lililotolewa na mkuu wa idara ya fedha/uhasibu anayewajibika kutayarisha taarifa za fedha za taasisi husika.

Ni wajibu wa Mhasibu kuisaidia Bodi wa Wakurugenzi/Bodi ya Uongozi kutekeleza wajibu wa kutayarisha taarifa za fedha za taasisi zinazoonesha hali halisi ya fedha na matokeo kulingana na viwango vya uhasibu vya kimataifa na kulingana na matakwa ya kisheria ya utoaji taarifa za fedha. Wajibu kamili wa kisheria wa kutayarisha taarifa za fedha ni wa Bodi ya Wakurugenzi/Bodi ya Uongozi kama ilivyo katika maelezo ya wajibu wa Wakurugenzi katika ukurasa uliotangulia.

Mimi CPA Z.E. MKINGULE kwa niaba ya idara ya uhasibu ya UDOM SACCOS LTD ninakubali wajibu wangu wa kuhakikisha kwamba taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31.12.2025 zimetayarishwa kulingana na viwango vya uhasibu vinavyotumika na kulingana na matakwa ya kisheria.

Hivyo nathibitisha kwamba taarifa za fedha zinaonesha hali halisi ya fedha ya UDOM SACCOS kunako tarehe hiyo na kwamba zimetayarishwa kutokana na kumbukumbu za fedha zilizotunzwa vizuri.

Imesainiwa na: .....

Cheo: Mshauri wa Fedha Outsourced Head of Finance from Audit Firm

Namba ya uanachama wa NBAA FCPA - PP -1365

Tarehe: 24-06-2024

CPA Z.E.MKINGULE (FCPA-PP -1365)
Managing Partner
Lugalo Financial & Tax Consultants
Certified Public Accountants in Public Practice
P. O. BOX 2879 DODOMA
Email : zemkingule@yahoo.com
lugalo.consultants@gmail.com
Mobile : 0754 65 15 49

TAARIFA YA HALI YA FEDHA HADI KUNAKO TAREHE 31.12.2025

	JEDNA	31.12.2025 TZS	31.12.2024 TZS
RASILIMALI ZA CHAMA			
Fedha taslimu na usawa	2	387,387,038	42,952,389
Mikopo ya wanachama	3	6,322,513,776	6,152,736,259
Wadaiwa Wengine	4	31,728,181	28,414,251
Uwekezaji KCBL	5	34,552,793	34,552,793
Mali za kudumu	6A	49,136,137	50,285,937
Mali isiyoshikika	6B	9,550,001	9,550,001
Kodi ya mapato	7	1,379,666	7,849,739
JUMLA YA RASILIMALI ZA CHAMA		**6,836,247,592**	**6,326,341,369**
MTAJI NA DHIMA			
MTAJI			
Akiba ya lazima		204,732,718	194,154,018
Fungu la kukombolea Hisa		153,549,539	145,615,514
Fungu la Elimu		102,366,359	97,077,010
Fungu la madeni Mabaya		153,549,539	145,615,514
Bima ya Mikopo		211,350,640	176,105,640
Limbikizo la ziada		289,169,635	268,012,235
Jumla ya Mtaji		**1,114,718,431**	**1,026,579,932**
DHIMA			
Hisa za wanachama	8	858,539,204	642,219,686
Akiba za wanachama	9	4,421,529,359	4,221,444,372
Amana za wanachama	10	170,306,062	178,017,962
Wadai	11	270,178,191	257,556,291
Kodi iliyoahirishwa(deferred tax)	12	976,346	523,123
Jumla ya Dhima		**5,721,529,161**	**5,299,761,434**
JUMLA YA MTAJI NA DHIMA		**6,836,247,592**	**6,326,341,366**

JEDWALI NAMBA 1 HADI 20 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....
MWENYEKITI

24/06/2026
.....
TAREHE

.....
MENEJA

24/06/2026
.....
TAREHE

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2025

MAELEZO	JEDNA	2025 TZS	2024 TZS
MAPATO			
Faida Riba juu ya mikopo		780,620,798	733,921,185
Toa Gharama za kifedha		220,000,000	220,000,000
JUMLA NDOGO		**560,620,798**	**513,921,185**
Mapato mengineyo	13	56,726,243	65,794,390
Mapato Bima BUMACO		452,438	-
Jumla ndogo		**57,178,680**	**65,794,390**
JUMLA YA MAPATO		**617,799,479**	**579,715,575**
MATUMIZI			
Gharama za Utumishi	15	83,348,231	89,177,527
Gharama za Utawala	16	425,127,336	393,310,491
Gharama za Biashara	17	21,933,329	23,140,358
JUMLA YA MATUMIZI		**530,408,896**	**505,628,376**
ZIADA KABLA YA KODI		**87,390,583**	**74,087,199**
TOA Tengo la kodi (30%)	18	(34,497,085)	(11,807,703)
ZIADA BAADA YA KODI		**52,893,499**	**62,279,496**

JEDWALI NAMBA 1 HADI 20 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....
MWENYEKITI

24/06/2026.
TAREHE

.....
MENEJA

24/06/2026
TAREHE

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KUNAKO TAREHE 31.12.2025

MAELEZO	AKIBA YA LAZIMA	AKIBA YA KUKOMBOLEA MAFUNGU	FUNGU LA ELIMU	AKIBA YA MADENI MABAYA	TENGO BIMA YA MAJANGA	LIMBIKIZO LA ZIADA	JUMLA YA MTAJI
	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS
	20%	15%	10%	15%			
Salio anzia 01.01.2024	181,698,119	136,273,590	90,849,060	136,273,590	142,115,660	243,100,437	930,310,456
Ziada/Hasara kwa mwaka						62,279,496	62,279,496
Matengo ya mwaka	12,455,899.20	9,341,924.40	6,227,949.60	9,341,924.40		(37,367,698)	
Marekebisho ya nyuma							-
Honoraria							
Bima ya mikopo					33,989,980		33,989,980
Salio ishia 31.12.2024	194,154,018	145,615,514	97,077,010	145,615,514	176,105,640	268,012,235	1,026,579,932

MAELEZO	AKIBA YA LAZIMA	AKIBA YA KUKOMBOLEA MAFUNGU	FUNGU LA ELIMU	AKIBA YA MADENI MABAYA	TENGO BIMA YA MAJANGA	LIMBIKIZO LA ZIADA	JUMLA YA MTAJI
	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS	TZS
	20%	15%	10%	15%			
Salio anzia 01.1.2025	194,154,018	145,615,514	97,077,010	145,615,514	176,105,640	268,012,235	1,026,579,932
Ziada/Hasara kwa mwaka						52,893,499	52,893,499
Matengo ya mwaka	10,578,700	7,934,025	5,289,350	7,934,025		(31,736,099)	-
Bima ya mikopo					35,245,000		35,245,000
Salio ishia 31.12.2025	204,732,718	153,549,539	102,366,359	153,549,539	211,350,640	289,169,635	1,114,718,431

JEDWALI NAMBA 1 HADI 20 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

MWENYEKITI

24/06/2026.

TAREHE

MENEJA

24/06/2026

TAREHE

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KUISHIA TAREHE 31:12:2025

	2025 TZS	2024 TZS
MTIRIRIKO WA FEDHA TOKA SHUGHULI ZA UENDESHAJI		
Mapato kabla ya kodi	87,390,583	74,087,199
Uchakavu	6,149,800	5,165,799
Tengo la mikopo mibaya	22,060,199	(13,472,361)
Fedha ingia/(toka kabla ya mtaji unaozunguka)	**115,600,582**	**65,780,637**
Mabadiriko ya Mtaji uzungukao		
(Kuongezeka)/kupungua kwa mikopo kwa Wanachama	(191,837,716)	(698,470,329)
Kuongezeka/(kupungua) kwa Amana za Wanachama	(7,711,900)	28,216,832
Kuongezeka/(kupungua) kwa Akiba za Wanachama	200,084,987	523,712,581
(Kuongezeka)/kupungua kwa Wadaiwa wengine	(3,313,930)	(902,600)
Kuongezeka/(kupungua) kwa wadai wengine	12,621,900	14,252,034
JUMLA NDOGO	**9,843,340**	**(133,191,482)**
Kodi iliyolipwa	(27,573,788)	(47,851,515)
JUMLA NDOGO	(17,730,448)	(181,042,997)
Fedha halisi/Tumika kwa shughuli za Uendeshaji	**97,870,134**	**(115,262,360)**
MTIRIRIKO WA FEDHA TOKA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI		
Ununuzi wa Mali za Kudumu	(5,000,000)	(10,150,000)
Fedha halisi toka/tumika kwa shughuli za Uwekezaji	**(5,000,000)**	**(10,150,000)**
MTIRIRIKO WA FEDHA TOKA SHUGHULI ZA FEDHA		
Kuongezeka/Kupungua kwa Hisa za Wanachama	216,319,518	91,952,028
Bima ya Mikopo	35,245,000	33,989,980
Fedha halisi toka/tumika kwa shughuli za kifedha	251,564,518	125,942,008
Ongezeko/Punguzo la fedha taslimu na usawa	344,434,652	529,648
Fedha na Vilinganisho vya Fedha Mwanzoni mwa Mwaka	42,952,386	42,422,740
Fedha na Vilinganisho vya Fedha Mwishoni mwa Mwaka	**387,387,038**	**42,952,388**

JEDWALI NAMBA 1 HADI 20 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....
MWENYEKITI
24/06/2026
.....
TAREHE

.....
MENEJA
24/06/2026
.....
TAREHE

JEDWALI ZA HESABU KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2025

JEDWALI NA 1.0 UTANGULIZI NA SERA ZA UHASIBU

1.1 UTANGULIZI

(a) **Kuandikishwa:**

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo UDOM kimeandikishwa tarehe 05.01.2011 chini ya Sheria ya Ushirika No 20 ya mwaka 2003 iliyofanyiwa marekebisho na kuwa sheria namba 6 ya mwaka 2013 na Nambari ya kuandikishwa ni DOR 715.

(b) **Madhumuni**

(i) Kupokea na kuweka akiba za wanachama wake kwa faida na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanachama wake

(ii) Kuwa ni njia mojawapo ya wanachama ya kujiwekea akiba.

(ii) Kuwaletea wafanyakazi huduma muhimu za kibenki na fedha karibu zaidi kwa njia ya akiba na mikopo.

(iii) Kuanzisha na kuendeleza shughuli zozote za kiuchumi kwa manufaa ya wafanyakazi wanachama kama itakavyokubalika na mkutano mkuu na kuidhinishwa na Mrajis wa vyama vya ushirika.

1.2 SERA ZA HISA

Hisa ni fedha za wanachama alizoweka chamani kama ni umiliki wake chamani, hisa ndiyo dhamana ya mwanachama na chama chenyewe uwekaji wa hisa utakuwa wazi kwa wanachama.

Thamani ya Hisa

Thamani ya hisa moja itakuwa shilingi elfu kumi (Tshs 10,000) na kiwango cha chini cha hisa ni hisa 5 (Tano) sawa na shilingi elfu hamsini tu (50,000)

1.3 SERA ZA AKIBA

Akiba ya fedha ambayo mwanachama ameweka chamani ikiwa ni dhamani ya kukopea au kuchukua kwa kutoa taarifa kabla ya kufanya hivyo. Akiba ndiyo itakayopima kiasi cha juu cha mkopo ambacho mwanachama anataka kukopa, ndiyo itakayoonyesha uwezo na nafasi ya kukopa.

1.4 Viwango vya akiba

Akiba ya mwanachama itaanzia kwa kima cha shilingi elfu kumi tu (Tshs 10,000) na hakuna kiwango cha mwisho cha kuweka akiba.

1.5 Thamani ya Akiba

Akiba ya wanachama itapokelewa kwa kiwango cha shilingi elfu kumi na thamani ya akiba itakuwa sawa na kiasi cha pesa kitakachokuwepo katika akaunti ya mwanachama.

1.6 SERA ZA AMANA

Amana ni fedha ambayo mwanachama ataweka chamani kwa mahitaji yake ya baadae na anaweza kuchukua wakati wowote wa masaa ya kazi ya chama.

Thamani ya Amana

i. Amana chini ya shilingi milioni hamsini haitawekewa faida.
ii. Riba ya asilimia nne (4%) itatolewa kwa akaunti ya amana yenye kuanzia shilingi elfu hamsini tu (50,000) na zaidi kwa mwaka.
iii. Hesabu ya riba itafanyika mwishoni mwa mwaka husika.

Kuweka Amana

Fedha zitawekwa na mtu yeyote katika akaunti kwa kujaza fomu maalumu ya kuweka fedha.

1.7 SERA YA MKOPO

Sera ya mkopo itatimiza madhumuni makuu ya chama ambacho ni kuinua hali ya uchumi na kijamii ya wanachama wake kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa kadri ya mahitaji yao na kufuata taratibu zilizowekwa na chama.

Ainaya mikopo (Huduma za mikopo)

Mikopo iliyopitishwa na chama ni kama ifuatayo:

i. Elimu
ii. Mikopo ya biashara
iii. Kilimo na ufugaji
iv. Mikopo ya thamani
v. Mikopo ya vyombo vya usafiri
vi. Mikopo ya ujenzi
vii. Mikopo ya kijamii
viii. Mikopo ya dharura kabla ya mwisho wa mwezi

Tengo la hasara

Endapo itatokea uchelewaji wa marejesho ya mikopo tengo la hasara litawekwa kulingana na muda na viwango kama ifuatayo:

a) Mikopo iliyocheleweshwa siku 31-90 itatengewa hasara ya 10% ya salio halisi la mkopo

b) mikopo iliyocheleweshwa siku 91-180 itatengewa hasara ya 30% ya salio halisi la mikopo iliyomashakani.

c) Mikopo iliyocheleweshwa siku 181-365 itatengewa hasara ya 50% ya salio halisi la mikopo iliyo mashakani.

d) Mikopo iliyocheleweshwa kwa zaidi ya siku 365 itatengewa hasara ya 100%.

1.8 MALI ZA KUDUMU

5036	Vikao vya Bodi, mikopo na kamati ya usimamizi	Chama kinatarajia kuwa na vikao 6 vya Bodi, vikao 12 vya kamati ya Usimamizi, vikao 24 vya kamati ya mikopo, vikao 6 vya menejimenti na vikao kazi 12. Vitakao hivi vitakaa kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali yahusuyo Chama.
5037	Mkutano Mkuu	Kwa mwaka 2027 Chama kinatarajia kuwa na mikutano mikuu miwili, utakayojumuisha wanachama takribani 1,000 kwa ajili ya kufanya maamuzi juu ya mambo mbalimbali yahusuyo Chama
5038	Posta na Simu	Tunakisia kutumia Tsh 350,000.00 kwa ajili ya ada ya sanduku la posta kwa mwaka 2027
5039	Usafi wa ofisi	Kwa mwaka 2027 tunategemea kutumia kiasi cha shilingi 3,000,000.00 kwaajili ya kumlipa mfanya ushafi pamoja na kununua madawa na sabuni za kufanyia usafi wa ofisi.
5040	Sherehe za kitaifa	Kwa mwaka 2027 Chama kinataraji kutumia Tsh 39,500,000.00 katika shughuli mbali mbali za ushirika ikiwemo sherehe za siku ya ushirika Duniani na siku ya Saccos Duniani, ACCOSCA pamoja na jukwaa la ushirika.
5042	Elimu na mafunzo kwa Wanachama	Tunakadiria kutumia Tsh 48,466,093.35 kutoa mafunzo na semina kwa wanachamai ili kuboresha na kuimarisha Chama chetu. Chama kinatarajia kuwapatia wanachama mafunzo kwa awamu mbili kwa mwaka 2027.
5041	Gharama za kuajiri	Chama kinatarajia kutumia kiasi cha Tsh 2,130,000.00 kwaajili ya ajira ya mkaguzi wa ndani katika kipimdi cha mwaka 2027
5043	Elimu na mafunzo kwa Bodi	Tunakadiria kutumia Tsh 24,233,046.67 kutoa mafunzo na semina kwa wajumbe wa Bodi na kamati ya usimamizii ili kuboresha na kuimarisha Chama chetu. Washiriki watalipwa Tshs 80,000/= ndani ya jiji. Nje ya mkoa italipwa nauli kulingana na umbali anaosafiri na posho ya kujikimu kwa siku Tshs 150,000/= kwa wajumbe Pia watalipwa Tsh 20,000/= kwa siku kwaajili ya usafiri wa ndani.
5044	Maboresho ya miundo mbinu ya ofisi	Ofisi inatarajia kutumia kiasi cha Tsh 1,200,000.00 kwa mwaka 2027 kwaajili ya maboresho ya mifumo ya umeme na internet pindi itakapo pata itilafu.
5045	Gharama za utengenezaji wa mfumo	Ofisi inatarajia kutumia Tsh 15,000,000.00 kutengeneza mfumo kwaajili ya utunzaji na uchakataji wa taarifa za chama na wanachama kwa mwaka 2027
5046	Uendeshaji mfumo wa taarifa	Kwa mwaka 2027 tunatarajia kutumia kiasi cha Tsh 2,870,000.00 kwaajili ya usimamizi na uendeshaji wa mfumo wa taarifa za Chama.

5047	Chai ya ofisi	Kwa mwaka 2027 tunatarajia kutumia kiasi cha tsh 4,920,000.00 kwajili ya matumizi ya chai kwa watendaji wa Chama.
5048	Matengenezo ya vifaa vya Ofisi	Matengenezo ya vifaa vya Ofisi (Computer, Printer, Photocopy machine, n.k), kwa mwaka 2027 tunategemea kutumia jumla ya Tsh 3,200,000.00
5050	Kodi ya kiwanj acha chama	Chama kinatarajia kutumia kiasi cha Tsh 300,000.00 kwaajili ya malipo ya kodi ya kiwanja kwa mwaka 2027
5051	Malipo kwaajili ya wafanyakaji wanaojitolea	Chama kinatarajia kutumia kiasi cha Tsh 4,800,000/= kwaajili ya kuwalipa wafanyakazi watakaokuwa wanajitolea katika ofisi za chama.

5053	Mchango kwa jamii	Kwa mwaka 2027 chama kinatarajiw kutumia kiasi cha Tsh 6,000,000.00 kwaajili ya kuijali jamii kama msingi namba 7 wa ushirika unavyo elekeza.
GHARAMA ZA BIASHARA 5060		
5061	Gharama za benki	Gharama hizi zitahusu gharama za kuomba bitabu vya cheki kwa mwaka, gharama za kuchakata malipo mbali mbali na gharama nyingine zitakazohusu benki
5062	Ada ya ukaguzi na gharama za ukaguzi	Tunakisia kuwalipa wakaguzi wa nje wa mahesabu Tsh 8,000,000.00 kwa kukagua Hesabu za mwaka 2026.
5063	Gharama za ufuatiliaji madeni	Kutokana na Chama kufungua mfungamano kwa kuendelea kuwa na wanachama walio hamishwa toka UDOM n.k, gharama za ufuatiliaji wa wanachama hao utaongezeka hivyo tunakadiria kuwa na gharama za ufuatiliaji makato, ambapo kila mfuatiliaji mmoja atalipwa Tsh 30,000/= malipo yatafanyika tu pale thamani ya ukusanyaji itakuwa umeridhisha, malipo haya yamejumuisha gharama za usafiri na chakula. Pamoja na ufuatiliaji wa dhamana za wanachama watakaoomba mkopo. Gharama hizi zimekadiriwa kuwa Tsh 9,000,000/= kwa mwaka 2027.
5064	Matangazo na machapisho	Tunakisia kutumia pesa hizi kwa ajili ya matangazo mbalimbali kampeni za kutangaza shughuli za Chama na uhamasishaji watu kujiunga na UDOM SACCOS LTD. Ikiwa ni kuchapisha vipeperushi na kutengeneza diary Pamoja na motisha kwa atakayeleta nwanachama mpya
5066	Gharama za Kandarasi/ Mifumo/ Sera	Tunakadiria kutumia Tsh 9,500,000.00 kwa shughuli za ushauri wa mambo mbalimbali kama Malipo ya washauri juu ya namna ya ukadiriaji kodi, mifumo na ukaguzi wake pamoja na TEHAMA.
5067	Vikao vya ukaguzi	Chama kinatarajia kuwa na vikao viwili vya ukaguzi kwa mwaka 2027 yani kipindi wakaguzi wanaanza kukagua na pindi watakapo maliza kukagua.
GHARAMA ZA UTUMISHI 5090		
5091	Mishahara ya watendaji	Chama kinatarajia kutumia kiasi cha Tsh 97,680,000.00 kwaajili ya kuipa mishahara pamoja na malimbikizo kwa mwaka 2027 kwa watendaji wake sita.
5092	Michango ya pensheni	Kwa mwaka 2027 Chama kinatarajia kulipa michango ya pensheni kwa waajiliwa wake saba, ikiwa ni 10% ya mishahara yao kwa mwaka sawa na shilingi 9,768,000.00
5093	Workers Compensation Fund (WCF)	Kwa mwaka 2027 chama kitalipa kiasi cha Tsh 511,200.00 WCF kutokana na mishahara ya mwaka 2027 ambapo Chama kitachangia 0.5% ya mishahara na posho za mwezi.

5094	Malipo ya Kodi ya SDL	kwa mwaka 2027 hakutokuwa na malipo ya SDL kwakuwa watendaji wetu hawajafika 10 kama sheria inavyoelekeza.
5095	Sare za Watendaji	Tunategemea kuwanunulia Sare Wafanyakazi saba kwa mwaka 2027 ili kuendelea kuwafanya wafanyakazi wa ofisi kuwa nadhifu na vitambulisho vya wafanyakazi, kiasi cha Tshs. 3,000,000.00 kwa mwaka, watendaji 6 @ 500,000/=
5096	Rambi rambi	Chama kimekisia kuwagharamia watendaji matukio ya msiba kiasi cha Tshs. 3,000,000.00 Walengwa ni Mtendaji mwenyewe, Baba mzazi, mama mzazi, mke, mume na mtoto wa watendaji kwa mujibu wa sera zetu.
5097	Malipo ya muda wa ziada	Endapo itatokea kuna umuhimu wa mtendaji kufanya kazi kwa muda wa ziada atalipwa kiasi cha Tsh 20,000.00 kwa siku za kawaida na Tsh 30,000.00 kwa siku za mapumziko na sikukuu.
5098	Elimu na mafunzo kwa Watendaji	Chama kinakadiria kutumia Tsh 24,233,046.67 kutoa mafunzo na semina kwa watendaji ili kuboresha na kuimarisha Chama chetu. Watendaji watalipwa Tsh 80,000.00 posho ya siku kwa ndani ya jiji. Nje ya mkoa italipwa nauli kulingana na umbali anaosafiri na posho ya kujikimu kwa siku Tshs 150,000/=. Pia watalipwa Tsh 20,000/= kwa siku kwaajili ya usafiri wa ndani.
5099	Malipo ya tahadhari ya kihasibu	Tunatarajia kuwa na malipo ya tahadhari za kihasibu kwa watunza fedha wa Chama ili kuweza kufidia pindi hatari inapoweza jitokeza, malipo haya yatalipwa kwa mwezi kiasi cha Tsh 40,000/= sawa na Tsh 960,000/=
5100	Bima ya Afya	Tunategemea kuwalipia watendahi wetu saba mfuko wa Bima ya Afya NHIF kwa mwaka 2026 kiasi cha tsh 2,930,400.00 kwa mwaka ili kuweza kuwahakikishia usalama wa afya zao pindi wawapo kazini ama sehemu wanazo ishi.
5101	Gharama ya kukaimu madaraka	Gharama hizi zitalipwa kwa wafanyakazi watakao kaimu nafasi za kazi kwa muda utakaozidi siku 14 za kazi, malipo haya ni tofauti ya mshahara wa mtu aliyekaimishwa na anae mkaimu.
5102	Posho ya madaraka (Responsibility allowance)	Malipo haya yatalipwa kwa Meneja na Mhasibu wa Chama. Pia watu hawa hawatolipwa malipo ya muda wa ziada kwa kuwa wao wanaweza kufanya kazi kwa masaa mengi Zaidi nje ya muda wa kazi.

AJENDA NA: 8

KUSOMA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BODI KWA MWAKA 2026

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA
(UDOM SACCOS LTD)

TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI
MAENDELEO NA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA CHAMA

KWA KIPINDI CHA MWAKA 2026

Imetayarishwa na:
Bodi ya Chama,
UDOM SACCOS LTD
P.O.Box 2765
Dodoma.
Barua pepe: info@udomsaccos.co.tz

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Wajumbe wa mkutano mkuu

Ndugu Wajumbe wa Bodi na kamati ya usimamizi

Ndugu Maafisa ushirika kutoka ofisi ya Mrasjis Msaidizi Mkoa

Ndugu maafisa ushirika kutoka ofisi ya Ushirika Jiji

Ndugu Wakaguzi kutoka ofisi ya ukaguzi COASCO

Ndugu wageni waalikwa wote

Kwanza kabisa napenda kumshukuru mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima na kutufanya tukutane tena siku ya leo ili tujadili maendeleo ya chama chetu. Nichukue fursa hii kuwashukuru wajumbe wenzangu wa bodi, kamati ya usimamizi, watendaji wa chama pamoja na wanachama wote kwa ujumla ambao tumekuwa nao sambamba katika kuhakikisha malengo ya chama chetu yanafikiwa.

2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA CHAMA

Ndugu wanachama, chama chetu kimekuwa kikitekeleza shughuli zake kupitia Bodi na Menejimenti kwa kuzingatia masharti ya chama, sheria za vyama vya ushirika pamoja na miongozo mbalimbali inayotolewa na Tume ya maendeleo ya ushirika, chini ya Mrajis wa vyama vya ushirika nchini.

Kwa mwaka 2026 chama chetu kupitia Bodi na menejimenti kimeweza kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo;

2.1 Kuongeza Wanachama Wapya

Kwa mwaka 2026 chama kilikadiria kuongeza wanachama wapya 100.

Utekelezaji

Katika kipindi cha mwezi Octomba, 2025 hadi Septemba, 2026 chama kimepokea wanachama wapya 21.

2.2 Ukusanyaji wa Mapato ya Chama

Kwa mwaka 2026 chama kilikadiria kukusanya kiasi cha Tsh 936,406,987.48 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

Utekelezaji

Katika kipindi cha mwezi Januari,2026 hadi Septemba,2026 chama kimefanikiwa kukusanya mapato kiasi cha Tsh 663,091,847.97 sawa na asilimia 94.42% ya lengo la kukusanaya Tsh 702,305,240.61 kwa miezi 9

Mchanganuo wa makusanyo kwa kipindi cha mwezi Januari, 2026 hadi Septemba, 2026 ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini;

Jedwali Na.1

Kasma	Chanzo cha mapato	Makadirio ya miezi 9	Halisi hadi Sept 2026	Asilimia ya utekelezaji
4010	Faida ya mikopo	648,076,490.61	619,508,938.00	95.59%
4011	Ada ya fomu	1,203,750.00	870,000.00	72.27%
4012	Ada ya mkopo	44,775,000.00	24,147,700.00	53.93%
4013	Viingilio	7,500,000.00	1,300,000.00	17.33%
4014	Adhabu	0.00	16,401,459.97	
4017	Mapato ya uwakala wa bima	750,000.00	863,750.00	115.17%
JUMLA		**702,305,240.61**	**663,091,847.97**	**94.42%**

2.3 Ziada kabla ya Kodi

Ndugu Wajumbe katika mwaka wa fedha 2026, Chama kilikadiria kupata ziada kabla ya kodi ya Tsh 154,347,582

Utekelezaji.

Katika kipindi cha miezi tisa Januari hadi Septemba 2026, Chama kimetengeneza faida kabla ya kodi Tsh 202,092,271 sawa na asilimia 174.58% ya makadirio ya Tsh 115,760,686.35 ya miezi tisa.

Jedwali namba 2 hapo chini linafafanua faida iliyopatikana katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2026

Jedwali Na. 2

MAELEZO	MAKADIRIO JANUARI - SEPTEMBA	HALISI HADI SEPTEMBA 2026	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI
Mapato	702,305,240.61	663,091,847.97	94.42%
Matumizi	586,544,554.26	460,999,576.59	83.68%
Faida	**115,760,686.35**	**202,092,271**	**148.80%**

3.0 Ukusanyaji wa Hisa, Akiba na Amana kwa kipindi cha mwezi Januari 2026 hadi Septemba 2026

Ndugu Wajumbe kwa mwaka 2026, Chama kimefanikiwa kukusanya fedha za hisa, akiba na amana kutoka kwa wanachama zenye jumla ya Tsh 441,646,992.58

Jedwali Na.3

MAELEZO	MAKUSANYO KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI - SEPTEMBA 2026
Hisa	52,064,557.07
Akiba	241,791,657.91
Amana	147,790,777.60
JUMLA	**441,646,992.58**

4.0 Utoaji na urejeshaji wa Mikopo ya wanachama kwa kipindi cha Mwezi January 2026 hadi Septemba 2026

4.1 Utoaji wa mikopo.

Ndugu Wajumbe, kwa mwaka 2026 chama kilikadiria kutoa mikopo ya Tsh 8,055,000,000 kwa wanachama wenye sifa za kukopeshwa.

Utekelezaji.

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2026, Chama kimeweza kutoa mikopo 600 yenye thamani ya Tsh 4,514,834,000.00 sawa na asilimia 74.73% ya makadirio ya Tsh 6,041,250,000.00 ya miezi tisa. Kwa ufafanuzi zaidi rejea Jedwali hapo chini.

Jedwali Na.4

MAELEZO	MAKADIRIO JANUARI HADI SEPTEMBA 2026	HALISI JANUARI HADI SEPTEMBA 2026	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI
Mikopo iliyotolewa 2026	6,041,250,000.00	4,514,834,000.00	74.73%

4.2 Urejeshaji wa Mikopo

Ndugu wajumbe mwaka 2026, Chama kilikadiria kukusanya marejesho ya Tsh 5,636,689,586.45 kutoka kwa Wanachama watakaokopeshwa.

Utekelezaji.

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2026, chama kimekusanya jumla ya Tsh 3,753,994,889.69 sawa na asilimia 88.8% ya makadirio ya Tsh 4,227,517,189.84 ya miezi tisa.

ufafanuzi zaidi rejea jedwali hapo chini;

Jedwali Na.5

MAELEZO	MAKADIRIO JAN - SEPT 2026	HALISI JAN - SEPT 2026	ASILIMIA
Marejesho ya mikopo ya 2026	4,227,517,189.84	3,753,994,889.69	88.8%

Kwa sasa kasi ya ukusanyaji wa marejesho imeongezeka kutokana na chama kuwa na uhusiano mzuri na benki ya CRDB ambapo wanachama wengi mishahara yao inapita.

Chama kimeendelea kushikilia akaunti za wanachama wasumbufu katika urejeshaji hadi pale marejesho yatakapo patikana kama mkataba wa mkopo unavyo sema.

5.0 Ongezeko la Mtaji tete na Mtaji Taasisi wa Chama.

5.1 Mtaji tete

Ndugu Wanachama kwa mwaka 2026 Chama kimefanikiwa kuongeza mtaji tete kwa Tsh 336,470,400.41 kutoka Tsh 1,978,857,633.59 mwaka 2025 hadi Tsh 2,315,328,034 Septemba mwaka 2026.

Jedwali hapa chini linafafanua zaidi

Jedwali Na. 6

MAELEZO	KIASI (TSH)
Hisa	939,906,235
Matengo yote ya kisheria.	991,059,897
Malimbikizo ya faida / hasara.	384,361,902
Misaada	0.00
JUMLA YA MTAJI TETE	**2,315,328,034**

5.2 Mtaji Taasisi

Pia kwa mwaka 2026 Chama kimefanikiwa kuongeza mtaji taasisi kwa Tsh 255,103,369.41 kutoka Tsh 1,120,318,429.59 mwaka 2025 hadi Tsh 1,375,421,799Septemba mwaka 2026.

Jedwali hapa chini linafafanua zaidi

Jedwali Na. 7

MAELEZO	KIASI (TSH)
Matengo yote ya kisheria.	991,059,897
Malimbikizo ya faida / hasara.	384,361,902
Misaada	0.00
JUMLA YA MTAJI TAASISI	**1,375,421,799**

6.0 Usimamizi na Ukaguzi wa Chama

Chama kimeweza kukaguliwa na COASCO na taarifa imesomwa kwenye mkutano Mkutano mkuu huu kupitia ajenda Na. 6

Aidha, Kamati ya Usimamizi iliweza kukagua utekelezaji wa shughuli za chama na kuandaa taarifa yake ambayo itasomwa kwenye mkutano mkuu huu kupitia ajenda Na.9

7.0 MAFANIKIO

Ndugu Wanachama katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2026 chama kimefanikiwa kufanya yafuatayo;

i. Kushiriki katika sherehe za siku ya Ushirika Duniani (SUD), Jukwaa la Ushirika Mkoa, ACOSCA, SACCA na semina mbalimbali za Viongozi wa Bodi, Watendaji, Kamati ya usimamizi na wanachama ikiwa ni kwa mujibu wa sheria za Ushirika na miongozo ya Mrajis.
ii. Chama kimefanikiwa kuwalipia ada na gharama zingine wanafunzi wanafunzi watano (5) kutoka Chuo kikuu cha Dodoma kiasi cha Tsh 4,020,500.00 kupitia program ya huduma kwa jamii inayo fanyika kimkoa kila mwaka.
iii. Chama kimefanikiwa kutoa mafunzo kwa wanachama 299 kupitia mpango wa utolewaji mafunzo kwa wanachama wa vya ushirika katika Jukwaa la ushirika Mkoa wa Dodoma mwaka 2026.

iv. Chama kimefanikiwa kuanza kuunda mfumo wa taarifa za chama utakao weza kurahisis ha shughuli za uchakataji na utolewaji wa taarifa za chama kwa wanachama na wadau wa chama.

v. Chama kimefanikiwa kufanya bonanza la kusherehekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwa UDOM SACCOS LTD

vi. Chama kimeweza kutoa mikopo kwa wanachama wake kwa wakati

vii. Chama kimefanikiwa kusimamia na kuhakikisha kinakuwa na ukwasi imara wakati wote wa kutoa huduma kwa wanachama.

viii. Tumefanikiwa kukusanya hisa kiasi cha Tsh 112,739,900.78 kutoka Tsh 825,048,552.26 Oktoba 2025 hadi Tsh 937,788,453 Septemba 2026 na

ix. Chama kimefanikiwa kuendelea kutoa riba juu ya akiba kwa wanachama wake.

8.0 CHANGAMOTO

Ndugu Wanachama, Chama kimekuwa kikikabiliana na changamoto zifuatazo;

i. Baadhi ya wanachama kucheleweshe marejesho.

Ombi: Bodi inaomba Mkutano Mkuu uazimie kufuta malimbikizo ya adhabu pamoja na riba kwa wanachama wanye madeni ya muda mrefu ili wapewe nafasi ya kulipa mkopo uliobaki.

ii. Kushindwa kuendeleza kiwanja cha chama, hali inayopelekea wananchi kufanya uharibifu kwa kuchimba mchanga kwenye kiwanja hicho.

Ombi: Bodi inaomba mkutano mkuu uazimie uendelezwaji wa kiwanja cha chama kwa kuweka ukuta utakaoweza kulinda usalama wa kiwanja hicho.

iii. Kuongezeka kwa tabia ya wanachama kuchukua akiba mara kwa mara

Ombi: Bodi inaomba wanachama waridhie pendekezo namba 1 hapa chini la uboreshaji wa akaunti ya Akiba na Amana.

9.0 MAPENDEKEZO YA BODI

Ndugu Wajumbe, Bodi inapendekeza mambo yafuatayo;

S/N	MAPENDEKEZO	SABABU	MATARAJIO
1	Uboreshaji wa akaunti ya Akiba na Amana ambapo mwanachama atachangia Tsh 50,000/= kama kawaida, lakini Tsh20,000/= itaingia kwenye Akiba na Tsh 30,000/= inaingia kwenye Amana. Mwanachama ataruhusiwa kuchukua Amana wakati wowote na kuitumia kama dhamana ya mkopo, lakini hatoruhusiwa kutoa Akiba ila ataruhusiwa kuitumia kama dhamana.	Itasaidia chama kuwa na ukwasi imara zaidi, na kupelekea kuongeza kiwango cha juu cha kukopa katika chama. Lakini pia itasaidia wanachama kukuza kiwango cha akiba kitakachopelekea kupata kiwango kikubwa cha mkopo pamoja na riba kubwa juu ya akiba mwisho wa mwaka	Kuongezeka kwa kima cha juu cha kukopa na kukua kwa ukwasi wachama
2	Kuongezeka kwa kiwango cha mkopo wa biashara hadi kufikia Tsh 50,000,000/=	Kuongeza mapato katika chama, na kukifanya chama kuwa na ukwasi imara	Kuimarika kwa ukwasi wa chama na kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa kukuza uwezo wa ndani wa kifedha.
3	Kuongezeka kwa kiwango cha mkopo wa chap chap hadi kufikia Tsh 1,000,000	Kuongeza mapato katika chama, na kukifanya chama kuwa na ukwasi imara	Kuimarika kwa ukwasi wa chama na kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa kukuza uwezo wa ndani wa kifedha
4	Kuongeza muda wa urejeshaji wa mkopo wa cha chap hadi kufikia miezi 6	Kumpa unafuu mkopaji katika urejeshaji wa mkopo wa chap chap	Kupunguza kiwango cha mikopo mibaya
5	Endapo pendekezo namba moja halitopita, bodi inapendekeza kupunguza vipindi vya uchukuaji wa akiba kwa mwaka kutoka mara nne hadi mara mbili kwa mwaka.	Kuongeza mapato katika chama, na kukifanya chama kuwa na ukwasi imara	Kuimarika kwa ukwasi wa chama na kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa kukuza uwezo wa ndani wa kifedha.
6	Kununua gari la chama kwaajili ya kurahisisha shughuli za chama.	Kuongezeka kwa huduma nje ya ofisi na kazi za chama	Kurahisisha utendaji wa kazi na huduma za chama

10.0 HITIMISHO.

Shukrani nyingi ziwaendee Wanachama wote, Watendaji, Ofisi ya Mrajis Msaidizi Mkoa, Ofisi ya Ushirika Jiji, Wakaguzi wa Shirika la COASCO na wadau wengine kwa ushauri na ushirikiano mkubwa mnaoutoa kwa Bodi ili kutekeleza majukumu yake.

Pia nipende kuwashukuru kipekee wageni wote waalikwa kwa kupokea mwaliko na kuhudhuria Mkutano huu mkuu wa UDOM SACCOS LTD. Bodi inaahidi kuyatekeleza yote yaliyoazimiwa na ingependa kuwaomba wanachama wote kila mmoja kwa nafasi yake kutimiza wajibu wake kwa wakati sahihi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza



Leonce S. Mujwahuzi
Mwenyekiti wa Bodi.
TAREHE 14/10/2026.

AJENDA NA: 9

KUSOMA TAARIFA YA KAMATI YA USIMAMIZI KWA MWAKA 2026

TAARIFA YA KAMATI YA USIMAMIZI YA UDOM SACCOS LTD KWA KIPINDI CHA OCTOBA 2025 HADI SEPTEMBA 2026

IMEWASILISHWA KWENYE MKUTANO MKUU WA 14 WA MWAKA, 2026

14 OCTOBA.

1. UTANGULIZI

Ndugu wanachama wa UDOM SACCOS LTD; awali ya yote napenda kutumia nafasi hii, kwa niaba ya Kamati ya Usimamizi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema hadi kufikia mkutano mkuu huu tangu tumalize mkutano wetu mkuu wa mwaka jana 2025.

Pia nitumie muda huu kuwashukuru wanachama wote kwa umoja na kwa ushirikiano wenu mnaoendelea kuuonesha kwetu kama viongozi wenu wa Kamati ya Usimamizi hadi kufikia siku ya leo.

Niwakaribishe wanachama wote mlioweza kuhudhuria katika mkutano wetu mkuu wa mwaka ambapo kwa pamoja tutajadiliana masuala mbalimbali na kufanya maazimio kadhaa kwa ajili ya ustawi wa chama chetu adhimu cha UDOM SACCOS LTD.

Katika muundo wa uendeshaji wa SACCOS, Kamati ya Usimamizi ni chombo muhimu kinachohakikisha uongozi wa chama (BODI) unatoa huduma bora kwa wenye chama chao bila upendeleo wala ubaguzi ili kufikia malengo waliyojiwekea ya kuleta ustawi kwenye maisha yao.

Kamati ya Usimamizi ina wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa shughuli kuu za chama, hususani kupokea ***hisa, akiba, amana, viingilio*** pamoja na ***kutoa huduma za mikopo*** na ***kukusanya marejesho ya mikopo*** **hiyo** kutoka kwa wanachama zinafanyika kwa weledi na ufanisi mkubwa na kwa kuzingatia **Sera**, **sheria**, **kanuni**, **miongozo**, mpango mkakati, **taratibu** na **maazimio** ya chama. Hii ni pamoja na uongozi wa chama kuhamasisha na kushawishi wafanyakazi wengi zaidi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kujiunga na chama chetu.

Ndugu wanachama Ili kufanikisha jukumu hili, Kamati hufanya kaguzi zake za kila baada ya robo ya mwaka (miezi mitatu mitatu) na mara nyingine kamati hufanya ukaguzi wa kushtukiza pale kamati inapohisi kuna utendaji usioridhisha kwa watendaji na kutoa ushauri kwa bodi ya chama kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa chama kinatoa huduma bora, na haraka kwa wanachama wote na kwa usawa ili pasiwepo na malalamiko kwao.

Ndugu wanachama taarifa hii inalenga kuelezea majukumu mbalimbali yaliyofanywa na Kamati ya Usimamizi kwa kipindi chote cha Oktoba 2025 hadi Septemba 2026, na kutoa taswira nzima ya maendeleo na mwelekeo wa chama chetu kwa siku za usoni kwa wanachama.

Hivyo kwa maelezo ya hapo juu, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo;

i. Kazi zilizofanywa na Kamati ya Usimamizi kuanzia Oktoba 2025 hadi Septemba 2026,
ii. Changamoto zinazoikabili Kamati ya Usimamizi,
iii. Ushughulikiaji wa malalamiko ya wanachama, na
iv. Hitimisho na mapendekezo kwa wanachama.

2. KAZI ZILIZOFANYWA NA KAMATI YA USIMAMIZI 2025 - 2026

Katika kipindi cha Oktoba 2025 hadi Septemba 2026, Kamati ya Usimamizi yenye wajumbe watatu imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa misingi ya sera, sheria, miongozo, kanuni na kwa kuzingatia taratibu za vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) kwa kufanya kaguzi katika maeneo mbalimbali ya chama kiutendaji.

Baadhi ya maeneo hayo ya kiutendaji yaliyofanyiwa ukaguzi ni pamoja na;

i. Utendaji kazi wa viongozi wa BODI na menejimenti ya chama,
ii. Utekelezaji wa maazimio ya mkutano mkuu wa kumi na tatu (13) wa mwaka 2025,
iii. Utekelezaji wa maoni ya kaguzi zilizopita za ndani (zilizofanywa na Kamati ya Usimamizi) na ukaguzi wa nje (uliofanywa na COASCO),
iv. Utoaji na urejeshaji wa mikopo, wadaiwa sugu na hatua zilizochukuliwa dhidi yao,
v. Utunzaji wa kumbukumbu ya mali za kudumu za chama,
vi. Mwenendo wa mapato na matumizi hadi Septemba 2025, na
vii. Taarifa za fedha (fomu za mikopo, hati za malipo n.k.

2.1. Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi (13) wa Mwaka 2025

Katika mkutano mkuu wa 13 wa mwaka 2025 wanachama kwa pamoja waliazimia maazimio nane (08) yaliyopaswa kutekelezwa na uongozi wa chama na kutolewa majibu ya utekelezaji wake kwenye Mkutano Mkuu wa 14, 2026.

Katika maazimio hayo yote kamati ya usimamizi_imefuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kubaini kutekelezwa kwa maazimio sita (06) na kubakia maazimio mawili (02) ambayo kamati ya usimamizi inayo taarifa ya utekelezaji wake kama ifuatavyo;

i) Manunuzi ya Viyoyozi kwa ajili ya ofisi ya chama.

Utekelezaji: Bodi inakusudia kununua viyoyozi hivyo kabla ya mwezi Disemba 2026.

ii) Wanachama wote waliochelewesha na wanadaiwa marejesho ya nyuma wapelekwe kwa Waajiri wao ili kuhakikisha fedha hizo zinarudishwa,

Utekelezaji: Bodi imewaandikia barua za kuwakumbusha kukamilisha madeni yao na iliwasiliana na mwajiri (DHRM - UDOM) kwa kuwasilisha majina ya wadaiwa hao kwa ajili ya kurejesha pesa wanazodaiwa na njia nyingine ni Bodi kufanya mawasiliano kwa njia ya WhatsApp kwa wadaiwa wote ambao hawakupatikana kukabidhiwa barua zao.

2.2 Utendaji wa Viongozi wa Bodi na Menejimenti

Kamati ya usimamizi imekuwa na utaratibu wa kufika mara kwa mara kwenye ofisi za chama kwa lengo la kukagua utekelezaji na utimizwaji wa majukumu ya chama kwa viongozi wa BODI na watendaji.

Pamoja na taarifa nyingine ambazo kamati inazitafuta na kujiridhisha na utendaji wao wa kazi ni kuangalia mahudhurio yao ya kila mara (kwa viongozi wa BODI) na mahudhurio ya kila siku (kwa watendaji) kwenye vitabu vya mahudhurio vilivyopo ofisini.

Utendaji wa viongozi wa BODI pamoja na watendaji kwa kipindi chote umekuwa wa kuridhisha.

2.3 Utekelezaji wa Maoni ya Kaguzi za Ndani na COASCO

Kamati ya usimamizi ilishiriki kwenye vikao vyote viwili vya COASCO kuanza ukaguzi na kumaliza ukaguzi wao.

Katika kikao cha kuhitimisha ukaguzi wao, COASCO walibaini kasoro baadhi za kiutendaji za wanachama kutokujaza fomu za mikopo kwa umakini na watendaji kusaini hizo nyaraka mbali mbali ilihali zinaonesha mapungufu ya ujazwaji.

COASCO walisisitiza umakini katika kuandaa nyaraka mbali mbali kwa ajili ya kuwa na kumbukumbu ya nyaraka sahihi chamani.

COASCO pia waliukosoa mfumo wa kidijitali wa kampuni ya ***fore site*** unaotumiwa na chama kutoa huduma kwa kusema una mapungufu mengi na unaweza kusababisha upotevu mkubwa wa pesa za chama. Mfumo hauna nywila imara inayoweza kutoa ulinzi wa uhakika wa pesa ya chama.

BODI ilishauriwa kuangalia upya matumizi ya mfumo huo na ikiwezekana kutafuta mfumo mwingine imara na madhubuti kwa ajili ya uhakika na usalama wa pesa ya chama. Kamati ya usimamizi ilikubaliana na ushauri huo ambao pia BODI iliuchukua kwa uzito mkubwa na sasa mfumo mpya unaendelea kujaribiwa katika awamu ya kwanza kuona ufanyajikazi wake ili unapokamilika wanachama waanze kuutumia.

2.4 Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo, Wadaiwa Sugu na Hatua zilizochukuliwa dhidi yao

2.4.1 Kamati ya usimamizi imefuatilia kwa karibu juu ya utoaji wa mikopo kwa wanachama.

Kwasasa utoaji wa mikopo mbalimbali ni wa haraka kutokana na Ukwasi wa chama kuimarika. Mikopo kwa wanachama inatolewa kwa kila juma kulingana na utaratibu uliowekwa na viongozi wa BODI ya chama baada ya uhakika wa upatikanaji wa pesa kwenye chama.

2.4.2Wakwapuaji Sugu

BODI kwa kushirikiana na menejimenti wamechukua hatua mbali mbali kufuatilia madeni kwa wakwapuaji sugu kama ifuatavyo;

i. BODI na Watendaji wamefanya vikao kadhaa na viongozi (Wakuu wa Idara) wa wanachama wakwapuaji sugu ili kuhakikisha pesa ya wanachama inarudishwa,

ii. BODI na menejimenti wamekuwa wakiwaandikia wadhamini wa wakwapuaji na kufanya nao vikao juu ya tatizo la wadhaminiwa wao kutokurejesha mikopo yao kwa wakati kama sheria inavyowataka,

iii. BODI na menejimenti wamechukua uamuzi wa kushikilia akaunti za wakwapuaji sugu wote ili kuhakikisha kila pesa yoyote inayoingia kwenye akaunti zao zichukuliwe na chama, na

iv. BODI na menejimenti wamefanya jitihada za kutembelea sehemu zao za biashara ili kujiridhisha na biashara zao na vipato vitokanavyo na biashara hizo kuweza au kutoweza kulipa madeni yao.

Hizi hatua zimesababisha ukwasi wa chama kuendelea kuimarika na kukiwezesha chama kuendelea kutoa mikopo kwa wanachama wake.

Kwa jitihada hizi za BODI na menejimenti wakwapuaji sugu kwa sasa wamepungua sana japo bado wapo ambao wamediriki kufanya vurugu kwa

mameneja wetu wa mabenki yetu yaliyoko UDOM bila kupita chamani ambako ndiko wangeweza kutatuliwa changamoto zao. Hivyo kamati inawaomba wanachama wote wenye tabia hizi kuacha mara moja na kurejea, kufuata na kuzingatia mikataba au masharti ya mikopo yao ambayo wamekubaliana nayo kwa maandishi.

2.5 Utunzaji wa Kumbukumbu ya Mali za Kudumu za Chama

Kamati ya usimamizi imekagua utunzaji wa kumbukumbu wa mali za kudumu za chama na kujiridhisha kwamba kumbukumbu za mali za chama zipo sahihi japo bado zipo mali za chama ambazo zimekwisha muda wake na zinatakiwa kuuzwa ila bado hazijauzwa.

Kumbukumbu za mali ya chama zinatakiwa kuendelea kuboreshwa kadri mali mpya za chama zinaponunuliwa.

2.6 Mwenendo wa Mapato na Matumizi hadi Septemba, 2026

Kamati imekuwa ikifuatilia kwa karibu mapato na matumizi ya chama na kubaini kuimarika kwa mapato ya chama. Hili limewezekana kwa jitihada kadhaa zilizofanywa na viongozi wa chama kama;

i. Ukusanyaji wa madeni toka kwa wanachama wasiowaaminifu kufanya marejesho, na

ii. Kupunguza muda wa kufanya marejesha kwenye mikopo ya maendeleo, dharura n.k.

2.7 Taarifa Za Fedha (Fomu Za Mikopo Na Hati Za Malipo)

Kamati ya usimamizi katika ukaguzi wake imefuatilia ujazaji wa nyaraka mbali mbali na kujiridhisha kutokuwa na upungufu wa kutokuzifanya hizo nyaraka kuwa halali.

Watendaji wanajitahidi kutimiza majukumu yao ya kila siku na kwa kuzingatia kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha (kwa watendaji wote wenye dhamana ya kusimamia fedha ya chama). Kamati ya usimamizi imeendelea kusisitiza umakini na kumaliza mapungufu madogo madogo yaliyoonekana kwenye nyaraka mbali mbali ili kuhakikisha kasoro zote zinamalizika.

2.8 Taarifa ya Uboreshaji wa Sera Mbali na Uandaaji wa Mfumo wa Kidijitali

Kamati ya usimamizi imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kwa msisitizo mkubwa kuhusu uboreshaji wa Sera mbali za chama.

Sera zilizotakiwa kufanyiwa maboresho na hatua zilizofikiwa ni kama zifuatazo kwenye jedwali hapa chini;

S/N	AINA YA SERA	HALI
1	SERA YA UWEKEZAJI	IMEIDHINISHWA
2	SERA YA UTUMISHI	IMEBORESHWA HAIJAIDHINISHWA
3	SERA YA ULINZI WA MLAJI	IMEIDHINISHWA
4	SERA YA UKAGUZI WA NDANI	IMEIDHINISHWA
5	SERA YA UHIFADHI KUMBUKUMBU	IMEIDHINISHWA
6	SEARA YA UHASIBU NA FEDHA	IMEIDHINISHWA
7	SERA YA UFUATILIAJI MADENI	IMEIDHINISHWA
8	SERA YA MIKOPO	IMEBORESHWA HAIJAIDHINISHWA
9	SERA YA MENEJIMENTI YA UKWASI	IMEIDHINISHWA
10	SERA YA UDHIBITI FEDHA HARAMU	IMEIDHINISHWA
11	MWONGOZO WA UDHIBITI VIHATARISHI VYA MAJANGA	IMEIDHINISHWA
12	MASHARTI YA CHAMA	IMEBORESHWA HAIJAIDHINISHWA
13	SERA YA MFUKO WA MAENDELEO	MPYA HAIJAIDHINISHWA
14	SERA YA MIGOGORO	MPYA HAIJAIDHINISHWA
15	SERA YA REHANI	MPYA HAIJAIDHINISHWA

16	SERA YA TEHAMA	MPYA HAIJAIDHINISHWA
17	SERA YA UUZAJI MALI	MPYA HAIJAIDHINISHWA

Kamati ya usimamizi pia imekuwa ikifuatilia kwa karibu utengenezwaji wa mfumo bora na rafiki wa kidijitali kwa matumizi ya chama na wanachama wake.

Kwa taarifa ya Bodi na watendaji mfumo upo kwenye hatua za mwisho kukamilika kwa ajili ya matumizi na kwenye mkutano huu wa 14, 2026 mtaalam wa IT wa chama ataufanyia majaribio kwa baadhi ya wanachama ili pamoja na mambo mengine ukafanyiwe marekebisho ya mwisho kwa matumizi ya chama.

3. CHANGAMOTO NA USHAURI KWA BODI

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Usimamizi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha ufanisi wa shughuli za ukaguzi na usimamizi wa chama. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

3.1 Kukosekana kwa Mkaguzi wa Ndani

Chama hakina mkaguzi wa ndani kwa miaka miwili sasa jambo ambalo limeongeza ukubwa wa kazi kwa kamati.

Ushauri:

a) BODI ifanye mchakato wa haraka ili kuajiri mkaguzi wa ndani ambaye ndiye jicho la karibu la kamati ya usimamizi ya chama kwa usimamizi wa shughuli za chama za kila siku,

b) BODI kutafuta wakaguzi wa chama wa "kuazima" kwa kipindi ambacho mchakato wa kupata mkaguzi wa ndani wa kuajiriwa unaendelea.

c) Bado kamati ya usimamizi inaisisitiza BODI ya chama **kuimarisha kamati ya mipango na fedha** itakayoshirikisha wajumbe wake na ikiwezekana

kujumuisha wanachama wenye taaluma ya mipango na fedha ili kuielekeza na kuisimamia menejimenti ya chama kwenye shughuli zote za chama. Kwani kamati hii ya mipango na fedha ndiyo ambayo itashirikiana na menejimenti ya chama kupitia mpango kazi na shughuli zote zilizoandaliwa kwenye mpango kazi wa chama.

Kamati ya usimamizi inaomba viongozi wote na menejimenti kushirikiana na kushikamana (kama inavyoonesha kwasasa) ili kudumisha mshikamano katika kuhakikisha chama kinafikia malengo yake kwa kutoa huduma iliyo bora zaidi na ya haraka kwa wanachama.

3.2 Uchukuaji wa akiba mara kwa mara

Kumekuwepo na changamoto ya wanachama kuchukua akiba zao mara kwa mara jambo linalosababisha chama kupunguza ukwasi na chama kukosa uweza wa kujiimarisha kimtaji.

Ushauri:

BODI kuja na mikakati ya kuhakikisha wanachama hawachuki akiba zao mara kwa mara ili kutunisha mfuko wa cahama.

3.3 Ufinyu wa bajeti ya kufanya ukaguzi

Kutokana na wingi wa bidhaa na huduma zinazotolewa na chama kwa wanachama, pamoja na ongezeko la taarifa zinazohitaji kupitiwa na kuhakikiwa, Kamati ya Usimamizi inahitaji muda wa kutosha ili kutekeleza majukumu yake kwa umakini na ufanisi.

Kwa sasa, kamati hutumia siku mbili kufanya ukaguzi na siku moja kuandaa taarifa ya ukaguzi. Hata hivyo, kutokana na ukubwa wa kazi na wingi wa taarifa

zinazopaswa kuchambuliwa, muda huo hautoshi kufanya ukaguzi wa kina katika maeneo yote yanayohitaji usimamizi.

Ushauri:

Kamati ya Usimamizi inaomba kuongezewa siku moja ya ziada kwa ajili ya shughuli za ukaguzi, ili kufikisha jumla ya siku tatu za ukaguzi, huku siku moja ikiendelea kutumika kuandaa taarifa ya ukaguzi. Hatua hii itasaidia kuongeza umakini, ubora na tija katika utekelezaji wa majukumu ya kamati.

Aidha, kamati inaomba kuzingatiwa kwa mahitaji ya bajeti yanayolingana na ukubwa wa majukumu yake ili kuwezesha utekelezaji wa ukaguzi kwa ufanisi zaidi.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Ndugu wanachama, kutokana na matokeo ya kaguzi mbalimbali ambazo zimefanywa na Kamati ya Usimamizi kwa kipindi cha oktoba 2025 hadi septemba 2026 pamoja na taarifa ya ukaguzi wa Nje uliofanywa na COASCO, Kamati inapenda kuwataarifu kuwa mwenendo wa chama chetu KIFEDHA na KIUTENDAJI ni wa kuridhisha na kamati itaendelea kusisitiza na kuomba kuimarisha utendaji bora zaidi kwa BODI na menejimenti ya chama.

Mwisho, naomba nichukue nafasi hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza wanachama wenzangu wote wa UDOM SACCOS LTD kwa ushirikiano wenu mnaoendelea kuutoa kwa Bodi, Kamati ya Usimamizi na menejimenti.

Ahsanteni kwa kuendelea kutuamini na tunaomba kupokea maoni toka kwenu kila mara panapoonekana pana uhitaji huo kwa lengo la kukijenga na kukiimarisha chama chetu.

Baada ya kusema hayo, ndugu wanachama wa UDOM SACCOS LTD naomba kuwasilisha.

"PAMOJA TUJENGE UCHUMI WETU"

Mwl. Meshack Kiburwi

Mwenyekiti

Kamati ya Usimamizi - UDOM SACCOS LTD

AJENDA NA:10
MABORESHO YA SERA NA MASHARTI

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA

(UDOM SACCOS LTD)

MABORESHO YA SERA KWA MWAKA 2026

Kwa mwaka 2026 chama kinatarajia kufanya maboresho katika Sera ya mikopo, ili kuongeza ufanisi katika utendaji pamoja na ubora wa bidhaa zinazotolewa na chama ili kukuza ukwasi.

Kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wa mkopo wa biashara kwa wanachama wetu, uongozi umefanya maboresho katika mkopo huo kwa kuongeza kiwango cha mkopo kutoka Tsh 30,000,000/= hadi kufikia Tsh 50,000,000/=

Pia wanachama wamekuwa na uhitaji mkubwa wa mikopo ya chap chap lakini wengi wamekuwa wakihitaji kuongezeka kwa kiwango cha mkopo huo. Hivyo Bodi imeona iongeze kiwango cha mkopo huo hadi kufikia Tsh 1,000,000.00 pamoja na muda wa marejesho kuongeza hadi miezi 6.

Aidha kutokana na akiba za chama kutotulia chamani hali inayoweza kukipelekea chama kukosa mtaji himilifu hapo baadae, Bodi imeandaa sera mpya kabisa ya uhamasishaji wa Hisa, Akiba na Amana ili kukijengea chama misuli ya mtaji na kukifanya kuwa himilivu katika soko la kiushindani.

Jedwali hapa chini linafafanua zaidi maboresho hayo

NB: Sera zingine mpya za kupitishwa zimeambatanishwa mwisho wa kabrasha hili

NA	MABADILIKO	NYARAKA INAYOBADILIKA	INAVYOSOMEKA SASA	ITAKAVYOSOMEKA BAADA YA MABADILIKO
1	Kuongeza kiwango cha juu cha mkopo wa biashara	SERA YA MIKOPO	**SURA YA SITA** **6.2 Ukomo wa Ukopeshaji kwa kila Aina ya Mkopo** Kiwango cha juu cha mkopo wa UDOM SACCOS Ltd bila kuathiri matakwa ya kanuni ya 33(1) ya kanuni za huduma ndogo za fedha - SACCOS itakuwa kama ifuatavyo. 2.Mkopo wa biashara Tsh 30,000,000/=	**SURA YA SITA** **6.2 Ukomo wa Ukopeshaji kwa kila Aina ya Mkopo** Kiwango cha juu cha mkopo wa UDOM SACCOS Ltd bila kuathiri matakwa ya kanuni ya 33(1) ya kanuni za huduma ndogo za fedha - SACCOS itakuwa kama ifuatavyo. 2.Mkopo wa biashara Tsh 50,000,000/=
		SERA YA MIKOPO	**SURA YA NANE** **8.8.1 Sifa na vigezo vya mkopo wa biashara** i. Mwanachama mfanyabiashara ataweza kupata mkopo wa Biashara mara tatu (3) ya akiba yake chamani hadi 30,000,000/= kulingana na aina na ukubwa wa Biashara	**SURA YA NANE** **8.8.1 Sifa na vigezo vya mkopo wa biashara** i. Mwanachama mfanyabiashara ataweza kupata mkopo wa Biashara mara tatu (3) ya akiba yake chamani hadi 50,000,000/= kulingana na aina na ukubwa wa Biashara
2	Kuongeza kiwango cha mkopo wa chap chap	SERA YA MIKOPO	**SEHEMU YA SITA** **6.2 Ukomo wa Ukopeshaji kwa kila Aina ya Mkopo** Kiwango cha juu cha mkopo wa UDOM SACCOS Ltd bila kuathiri matakwa ya kanuni ya 33(1) ya kanuni za huduma ndogo za fedha - SACCOS itakuwa kama ifuatavyo.	**SEHEMU YA SITA** **6.2 Ukomo wa Ukopeshaji kwa kila Aina ya Mkopo** Kiwango cha juu cha mkopo wa UDOM SACCOS Ltd bila kuathiri matakwa ya kanuni ya 33(1) ya kanuni za huduma ndogo za fedha - SACCOS itakuwa kama ifuatavyo.

			7. Mkopo wa ChapChap Tsh. 500,000/=	7. Mkopo wa ChapChap Tsh. 1,000,000/=
3	Kuongeza muda wa urejeshaji wa mkopo wa chapchap	SERA YA MIKOPO	**SEHEMU YA TANO** **5.0 Muda kikomo wa marejesho ya mkopo** **5.1 Ukomo wa Kurejesha Mkopo** Jedwali Na. 2 Chapchap muda wa marejesho – Hadi miezi 5	**SEHEMU YA TANO** **5.0 Muda kikomo wa marejesho ya mkopo** **5.1 Ukomo wa Kurejesha Mkopo** Jedwali Na. 2 Chapcha muda wa marejesho – Hadi miezi 6

AGENDA NA: 11

KUPITISHA MKAGUZI WA NJE WA HESABU ZA CHAMA ZA MWAKA 2026

AGENDA NA: 12

MENGINEYO

(KWARUHUSA YA MWENYEKITI)

AGENDA NA: 13

KUAHIRISHA MKUTANO